SUPA JACKPOT
TZS. 1,072,549,524
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Takwimu** ujauzito kwa wanafunzi zalishtua Bunge

UKURASA 3


Vita Russia, Ukraine huzuni kwa wajasiriamali kila kona
SMZ inakumbuka ahadi ya kurekebisha sheria kandamizi?
siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
MARTIN LUTHER KING: 'NINAYO NDOTO'
Maono yake yanavyobaki kuwa fikra inayoishi kwa wanasiasa, wanaharakati
CHONGOLO AONA FEDHEHA MORO
Viongozi, watendaji waangamiza vijiji kisa? Hongo za mifugo, fedha

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Februari 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581208

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### CHONGOLO ATOA SIKU 7 WIZARA KULIPA FIDIA



WIZARA ya Malisili na Utalii, imepewa siku saba kufika na...



UKURASA WA 4

### MO DEWJI AONGEZA AJIRA HADI 35,000

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo', ameongeza ajira...

UKURASA WA 8

### NURU KUMALIZA TATIZO MAJI DAR YANG'ARA



MWANGA wa kumaliza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani umeanza kuonekana kutokana na ujenzi wa Bwawa la Maji...

## Lema atangaza rasmi tarehe kurejea nchini

UKURASA 3

# Madudu Polisi, DPP, TAKUKURU

• **Imo** pia Tume ya Dawa za Kulevya, Rais aunda timu ya vigogo kuzichunguza... *Endelea ukurasa 2*





Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni



Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya



IGP Camillus Wambura



DPP, Sylivester Mwakitalu



# Mbunge aikaba koo serikali kupanda gharama za maisha

UKURASA 2

MICHEZO BALEKE AIWAHI SINGIDA BIG STARS UK.24 KATUNI UK.6

# Rais aibua madudu Polisi, DPP, TAKUKURU

**Na Restuta James**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amebainisha madudu mazito ndani ya Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na Tume ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kutokana na mfumo mbovu wa kiutendaji ambao umesababisha wananchi kuzilalamikia juu ya mwenendo mzima wa utoaji haki.

Amesema ndani ya taasisi hizo, kumekuwa na mmomonyoko wa maadili, upendeleo katika upandishaji vyeo, kuwabambikia watu kesi zikiwamo za uhujumu na dawa za kulevya. Amesema mambo hayo pamoja na mengine. Yamesababisha jamii kukosa imani na taasisi hizo hata kuzinyooshea vidole juu ya utendaji wao.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Rais ameunda tume ya kuangalia jinsi ya uboreshaji wa taasisi hizo huku akitaka ifanye tathmini ya kina juu ya utendaji na kutoa mapendekezo.

Akizindua tume hiyo inayooongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, jijini Dodoma jana, Rais Samia alisema tume hiyo pia itafanya tathmini ya utendaji wa Mahakama na Jeshi la Magereza kwa kipindi cha miezi minne kuanzia jana hadi Mei 30, mwaka huu.

Pia alisema mabalozi wanazoiwakilisha Tanzania nchi mbalimbali nao wamewekwa 'mguu sawa' kwa kuwa katika kipindi cha wiki tatu zijazo, ataunda tume ya kutathmini sekta ya mambo ya nje.

Akizungumzia ofisi ya DPP, Rais Samia aliitaka tume ibaini kasoro zilizoko kutokana na miaka ya karibuni kunyoshewa kidole na wananchi.

"Nyuma hapa kidogo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kulikuwa kuna ngoma kubwa kidogo inachezwa mpaka kukusanya fedha za wale wa 'plea bargaining'. zingine zimeonekana, zingine hazionekani.

"Uki-trace (ukifuatilia) utaambiwa kuna akaunti China sijui imepeleka fedha zipi. Kayatazameni haya yote, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuna nini hasa kilichoharibu hii ofisi," alisisitiza.

Kuhusu TAKUKURU, Rais Samia ameielekeza tume kutathmini kama watumishi wa taasisi hiyo wanapambana na rushwa au la.

"Huko ndani kuko kusafi kiasi gani? Twendeni tukatizame kwa sababu kubadilisha tu Mkuu wa Taasisi hakusaidii...akiingia anakuta mizizi imeota pale ya miaka na miaka lakini yeye kwa kuwa ni mpya watamdanganya tu," alisema.

Akizungumzia Magereza, aliitaka tume iangalie hali yake na kuja na mapendekezo ya maboresho kulingana matakwa ya karne ya 21 kwa kuainisha zilivyo na zinavyopaswa kuwa.



Aidha, kwa upande wa Jeshi la Polisi, limekuwa likizungumzwa vibaya na wananchi kuhusu utendaji wake wa kila siku. Rais alibainisha kuwa watu 70 kati ya 100, wanalizungumzia vibaya jeshi hilo lililopewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

**DAWA ZA KULEVYA**

Kuhusu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Rais Samia, alisema inahitajika tathmini ya utendaji kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya ubambikiaji wa dawa hizo haramu kwa watu wasio na hatia.

"Tumekuwa na kesi kadhaa, vijana wetu hawa wanakwenda kumtegeshea mtu halafu wanakwenda wanazunguka unaona kikundi cha watu kinakuja kukupekua kumbe wametegesha wenyewe," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Samia, kitendo hicho kinawabambikia kesi watu wasio na hatia na kuwaacha watuhumiwa wa biashara hiyo haramu wakiendelea na maisha.

Alisema nia yake ni kutengeneza mfumo ambao utalinda haki za watu kwenye ngazi zote za taasisi hizo.

**AHUENI MAHAKAMA**

Hata hivyo, alisema rushwa iliyokuwa imekithiri ndani ya mahakama imepungua baada ya maboresho mbalimbali yaliyofanywa. Hata hivyo, aliitaka tume hiyo kuangalia ni kipi kiongezwe au kipunguzwe ili kuboresha zaidi mfumo wa utoaji haki.

**HADIDU REJEA**

Tume hiyo yenye wajumbe 12 imepewa kazi ya kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa haki jinai na kutoa mapendekezo ya kufanya maboresho, ili kukidhi matakwa ya serikali na ya wananchi.

Tume hiyo imepewa hadidu rejea tano ambazo ni kuangalia utendaji wa taasisi hizo, mafunzo na ajira, mifumo ya ajira na upandishaji wa vyeo, matumizi ya Teknolojia na Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na fikra za kiutendaji kati ya taasisi hizo na wananchi.

Alitoa mfano wa matumizi ya TEHAMA kwamba katika karne ya 21, taasisi hizo zinapaswa kuwasiliana haraka kuanzia mtuhumiwa anapokamatwa, kuhojiwa hadi kufunguliwa kesi na kwamba mchakato mzima unatakiwa kutoa taarifa kwa mamlaka nyingine.

Aliitaka tume kutaja sheria au kifungu mahusisi itakachopendekeza kirekebishwe, ili kazi ya maboresho ifanywe haraka na taasisi zinazofanyiwa tathmini kutoa ushirikiano kwa tume hiyo ili kazi ikamilike kwa wakati.

**WAJUMBE WA TUME**

Wakati Jaji Chande akiteuliwa kuwa Mwenyekiti, Makamu wake ni Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue.

Wajumbe ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais (Utumishi), Dk. Laurean Ndumbaro, wakuu wa Jeshi la Polisi wastaafu Saidi Mwema na Balozi Ernest Mangu.

Wengine ni Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Edward Hosea, Askari Polisi mstaafu Saada Makungu, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Omar Issa, Ofisa Mwandamizi Ofisi ya Rais, Baraka Leonard na Mkurugenzi wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Zanzibar na Rais mstaafu wa Chama cha Wanasheria Zanzibar, Yahya Khamisi Hamad.

Kuhusu kuundwa kwa Tume ya kutathmini sekta ya mambo ya nje, Rais Samia alisema amekwishaongea na Katibu Mkuu Kiongozi na kwamba wanatarajia kuiunda katika kipindi cha wiki mbili hadi tatu zijazo.

Alisema pamoja na mambo mengine, tume hiyo itatathmini utendaji wa mabalozi na ikiwa wote wana sifa za kushika wadhifa huo.

# Gambo aikaba koo serikali kupanda gharama za maisha

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, ametaka serikali kuacha kujificha kwenye kichaka cha vita vya Ukraine, UVIKO- 19 na mabadiliko ya tabianchi kuhusu suala la kupanda kwa bei ya bidhaa na gharama za maisha.

Badala yake, ameiomba serikali iwaangalie wananchi kwa jicho la huruma kwa kuwa manung'uniko ni mengi.

Gambo aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akichangia taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na ile ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

"Tunafahamu kuna changamoto masuala yanayohusiana na mishahara, ukiangalia sekta binafsi mshahara wa kiwango cha chini umetoka kwenye 120,000 mpaka 140,000 kwa maana kuna ongezeko la Sh. 20,000.

"Kwenye sekta ya umma, tumetoka Sh. 300,000 mpaka Sh. 375,000 tumeongezewa 75,000. Ninasema hayo ili nitakapozungumzia mfumuko wa bei tuangalie na athari tulizo nazo kwenye maisha ya kila siku kwenye mishahara pamoja na changamoto mbalimbali," alisema.

Gambo alisema mtandao wa Wizara ya Kilimo, ambao umetoa takwimu mbalimbali kulingana na bei za vyakula, unaonyesha kwenye upande wa mchele, mwaka 2020 kilo moja ilikuwa Sh. 1,486 lakini mwaka 2023 kilo moja ni Sh. 2,888 ambayo ni bei ya jumla yua sokoni.

Alisema kwenye mahindi, bei imetoka Sh. 570 mwaka 2020 mpaka Sh.1,160 mwaka 2023 huku maharage ikitoka Sh. 2,400 mpaka 2,916.

"Mheshimiwa Spika ukiangalia hapa tu kwa mujibu wa maelezo ya Wizara ya Kilimo, mfumuko wa bei umesababishwa na sababu nne ambazo ni UVIKO-19, vita vya Urusi na Ukraine, kupanda kwa bei za mafuta na mabadiliko ya tabianchi.

"Kwa maoni yangu sababu zote hizi zimeangaliwa kutoka shambani hadi waliposafirisha hadi zikafika sokoni ndiyo maana leo bei imekuwa Sh. 2,888 kwa mchele, Sh. 1,160 kwa mahindi na 2,916 kwa maharagwe.

"Ukiacha bei ya jumla, ukienda kwenye soko lenyewe kwa maana ya bei ya rejareja, ukitembelea soko la Majengo hapa Dodoma, unakuta mchele unauzwa mpaka Sh. 3,400, ukienda Arusha Sh.3,500. Sasa ninajiuliza kutoka Sh. 2,888 kama wastani hadi kufika Sh. 3,500 jukumu la serikali ni nini?

"Sasa hivi wafanyabiashara kama wako huru sana kujiamulia kupanga bei wanavyotaka maana kutoka Sh. 2,888 mapaka Sh. 3,500, kuna tofauti kubwa. Mzigo mkubwa wa usafirishaji tayari umeshabebwa kutoka shambani mpaka sokoni. Mzigo wa pembejeo umeshabebwa, huyu anayetoa soko kuu Arusha au soko kuu la Majengo na kwenda kupeleka dukani kuuza rejareja kwa nini kuna tofauti kubwa? Hapa kuna kazi ya serikali kufanya ya kusimamia mfumuko wa bei na si kuacha bei ya kiholela kwenye maeneo mbalimbali," alisisitiza.

Jambo la pili, mbunge huyo alisema wakiangalia taarifa kwenye mtandao wa wizara, inawatia moyo wafanyabiashara kuendelea kuuza bidhaa bei ya juu.

"Ukiangalia mfano taarifa yao ya tarehe mbili mpaka sita Januari mwaka 2023, kwa upande wa Mkoa wa Dodoma wanatuambia kwamba mchele unauzwa mfano Sh. 3,400 kwa maana ya rejareja, lakini mhusika kule amenunua kwa Sh. 2,775 kuna ongezeko mara 625."

"Upande wa Arusha ukiangalia Sh. 4,000 lakini bei ya jumla amenunua Sh. 2,900 kwa hiyo kuna ongezeko mara 1,100. Kibaya zaidi ukiangalia Mkoa wa Kilimanjaro Wizara ya Kilimo inatwambia bei ya mchele sasa hivi kwa bei ya jumla ni Sh. 3,500, nikawa ninajiuliza Mheshimiwa Spika kama pale Arusha ninaweza kununua mchele kwa bei ya jumla Sh. 2,775 inakuwaje Kilimanjaro tunanunua kwa Sh. 3,500," alihoji.

"Ni rahisi sana kwa mwananchi kupanda daladala kutoka pale Kilimanjaro akalipa nauli Sh. 5,000 akafika Arusha akanunua mchele akarudi Kilimanjaro akatumia Sh. 10,000, lakini ukiangalia gharama ambayo imeongezeka hapa si chini ya Sh. 500 na zaidi.

"Unaona kabisa japo kuwa serikali imejificha kwenye vita ya Ukraine, kwenye uviko, mabadiliko ya tabia nchi, lakini bado kuna kazi ya kufanya ili kuondoa mfumuko wa bei kwenye maeneo mbalimbali," alisisitiza.

**MWIGULU AJIBU**

Baada ya maelezo hayo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alitoa taarifa kwamba serikali haijajificha kwenye vita vya Ukraine, UVIKO -19 wala mabadiliko ya tabianchi.

"Nimpe taarifa kwamba mambo ya Ukraine, ya UVIKO ni hali halisi ya dunia, si kisingizio. Haya ni mambo halisia na serikali imechukua hatua ambazo kwa Afrika Mashariki na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hakuna iliyochukua hatua hizo ya kutoa Sh. bilioni 100 kila mwezi kwa ajili ya kupunguza gharama ndiyo maana unaona hata nchi jirani wanakimbilia kuchukua vitu kutoka nchini kwetu," alisema.

"Nitoe taarifa pamoja na kwamba kuna jitihada zingine zinaendelea kuchukuliwa lazima tupongeze jitihada zilizokwisha fanyika na serikali ipo macho sana kwenye haya mambo na inaendelea kuchukua hatua."

Baada ya maelezo hayo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alipomuuliza Gambo kama anapokea taarifa hiyo, alisema, "Mimi siipokei kwa sababu ni wajibu wake kuitetea serikali, ninaomba nisiipokee nimpongeze kwa kazi yake nzuri ya kuitetea serikali."

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu nao watapata fursa ya kuchangia, itakuwa vizuri kuliweka vizuri jambo hilo kama alivyosema Waziri wa Fedha.

HABARI KITAIFA

# Lema atangaza rasmi tarehe kurejea nchini

Na Elizabeth Zaya

BAADA ya kimya cha muda mrefu, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, amesema atarejea nchini Machi Mosi, mwaka huu, kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Akizungumza katika mahojiano maaluma kwa simu na Nipashe jana, Lema alisema anarejea nchini si kwa sababu ya kauli ya serikali bali kwa kuwa amepata amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu kufanya hivyo kuja kuwatumikia wananchi na wafuasi wa chama chake kwenye kanda yake na nchi nzima kwa ujumla.

"Nimeshaamua kwamba nakuja nyumbani Machi Mosi, mwaka huu na nitatua KIA mchana, nitapokewa na wanachama wetu na wananchi na kanda nzima ya Kaskazini, nitakwenda kufanya mkutano wa hadhara mjini Arusha.

"Ninarudi nyumbani kwa sababu ya wito wa kuitumikia nchi yangu na huu wito umekuwa wa mkubwa zaidi kwa sababu nimepita kwenye uzoefu mbaya sana nilipotoroka nchini.

"Hakuna uzoefu mbaya katika maisha kama kukimbia nchi. Ni uzoefu mbaya sana ambao umeimarisha wito wangu mkubwa nilio nao kwa ajili ya kupigania utawala bora ili mtoto wa mtoto wangu, au mtoto wako wewe, au wajukuu wa nchi yetu wasije wakapita katika mambo tuliyopitia sisi," alisema Lema.

"Nilikimbia nchi kwa sababu ya kuhofia maisha yangu, sikukimbia nchi, sikukimbia chochote, nilikimbia kuhofia maisha yangu. Narudi nyumbani si kwa sababu ya (Hamad Yussuf) Masauni Bungeni (Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi). Narudi nyumbani kwa sababu ya amani niliyo nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

"Narudi kufanya kazi ya kutumikia nchi yangu ya kupigania demokrasia, haki na usawa kwa nguvu zangu zote kuliko wakati mwingine wowote, siji kuwa chawa, wala mpambe, nakuja kuikosoa serikali inapokosea na kuishauri inapohitaji ushauri.

"Kwa kipindi kifupi ambacho nimekaa hapa (Canada) naweza kusema kwamba nilikuwa natizama na kutafakari sana hao wenzetu wanafanyaje mpaka wamefika kwenye hatua waliyofika, naamini nitakuwa na mchango bora sana na chanya kwa jamii yangu," alisema.

Lema alisema anakuja kujipanga kuandaa wagombea ubunge, madiwani na viongozi wa serikali za mtaa, kata wa kanda anayoiongoza kupitia chama chake kwenye uchaguzi wa mwakani wa serikali za mitaa.

Aidha, aliwaomba wananchi na wafuasi wa chama hicho kwenye mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Tanzania yote kwamba hilo ndilo linalomrejesha.

**KUHUSU USALAMA WAKE**

"Hiyo amani kwa sasa nimeipata lakini siamini kwamba mazingira ni mazuri asilimia 100 sina huo ujasiri wa kuamini hivyo, kwa sababu waliompiga Tundu Lissu risasi hawajakamatwa, bado hatujamuona Ben Saanane, Azory Gwanda. Uhalifu unaweza kuwa bado uko ndani, lakini wakati mwingine unakuwa hauna uchaguzi zaidi ya kufanya kile kitu ambacho ni kigumu," alisema.

Lema alisema yako mambo ambayo yalikuwa yakimkwamisha kurejea nchini, ikiwamo ni kutokana na yeye kufungua biashara pamoja na kuendesha shughuli zake nyinginezo katika nchi hiyo kwa ajili ya kuendesha maisha.

## Takwimu za ujauzito kwa wanafunzi zalishtua Bunge

Na Augusta Njoji, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameagiza serikali kupeleka takwimu za watu waliokutwa na hatia kwa kuwapa ujauzito wanafunzi ili bunge liangalie kama sheria iliyopo inahitaji kuongezewa makali kukomesha vitendo hivyo.

Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 na 2022, wanafunzi wa shule za msingi waliopata ujauzito ni 1,554 na sekondari ni 7,457.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana bungeni baada ya Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, kujibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Hawa Mchafu, aliyehoji masuala ya wanafunzi waliopata ujauzito kurejeshwa shuleni.

Alisema takwimu hizo zitasaidia sana bunge kujua kama sheria inahitaji kurekebishwa ili kupunguza watu hao badala ya takwimu kuendelea kukua.

"Suala hili linahusiana na wizara yako na nyingine tutatamani kujua si leo kwa kuwa ni suala la takwimu. Hizi takwimu ni kubwa sana za ujauzito kwa shule za msingi na sekondari.

"Tungependa kujua kati ya hawa kwa sababu ni binadamu na hapa kila mmoja ni binti maana yake yupo aliyempa ujauzito kati ya hawa na wale waliowapa ujauzito ni wangapi wamechukuliwa hatua yaani yupi ambaye amekutwa na hatia huko mahakamani ili tujue kama sheria kweli inawalinda hao watoto na hivyo vitendo viovu au hapana," alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge Mchafu alihoji wanafunzi wangapi waliokuwa wajawazito na wangapi wamerejeshwa shuleni baada ya agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia katika swali la nyongeza, Mbunge alisema miongoni mwa sababu za wanafunzi kupata ujauzito wakiwa shuleni ni mazingira ya ukatili, unyanyasaji na umaskini uliokithiri kwenye maeneo wanayoishi.

"Serikali haioni sasa ni muhimu wasichana kuwaweka kwenye shule za mabweni ili kusoma kwa utulivu na kuondokana na mazingira yale? Agizo la kurejesha wasichana waliopata ujauzito shuleni linatekelezwa chini ya waraka namba mbili wa mwaka 2021. Kwa nini serikali isitunge sheria kuhusu suala hili ili asije kutokea kiongozi mwingine kubadili jambo hili lenye dhamira njema?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Kipanga alisema hadi Januari, mwaka huu, wanafunzi waliorejea shuleni baada ya kukatiza masomo kwa sababu ya ujauzito na kuendelea na masomo ya sekondari ni 1,692.

"Aidha, kwa upande wa elimu ya msingi, serikali inaendelea kukusanya taarifa za wanafunzi waliorejea shuleni baada ya kukatiza masomo kwa sababu ya ujauzito," alisema.


PRESS RELEASE

FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY

**''Foundation for Civil Society (FCS) Board of Directors'' Appoints New Board Members to join FCS Board**


Mrs **Mercy E. Sila**


Dr **Anthony Mveyange**


Mrs **Tertula M Swai**

**Dar es Salaam, 27th January 2023**. Foundation for civil society (FCS) board of directors is pleased to announce the appointment of three board members; Dr Anthony Mveyange, Mrs Mercy Sila, and Tertula Swali effective from 9 January 2023.

**Mrs Mercy Emmanuel Sila's** experience spans four decades in the workforce and has held previous high-level positions at Tanzania Education Authority (TEA), Tanzania Revenue Authority (TRA), Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC), and Tanzania Harbours Authority. She has also worked as the District Commissioner (DC) for Arumeru and Mkuranga Districts. Mrs Sila holds a Masters in Business Administration (MBA) from City University in London Majoring in Human Resources Management), a Post Graduate Accountancy Diploma from Nyegezi Social Training Centre (currently SAUT) in Tanzania, a Certified Public Accountancy (CPA (T) with National Board of Accountants and Auditors Tanzania (NBAA).

**Dr Anthony Mveyange** is the newly appointed Global Public Investment Lead for Africa for Development Initiatives, an INGO based in Nairobi, Kenya. He is currently transitioning out as the Executive Director of Partnership for African Social African Governance Research (PASGR) also based in Kenya. He holds a Ph.D in Economics and have extensive experience in designing and evaluating projects, programs, policy advisory, and research-related initiatives in Africa, and has worked for such organizations as the World Bank, United Nations World Institute for Development Economics Research, Trademark Africa, Porticus Africa, Amref Africa, and African Economic Research Consortium.

**Mrs Tertula M Swai** is an independent agribusiness and private sector development consultant with diverse competencies and skills in stakeholder consultation processes; programme management; establishing strategic partnerships with government authorities, civil society and private sector; economic and policy studies coordination with a gender focus; public-private dialogue facilitation; women's economic empowerment training and facilitation . Ms. Swai has held various posts with different capabilities in Agricultural Markets Development Trust (AMDT), UN Women Tanzania, Tanzania Private Sector Foundation (TPSF), Participatory Agricultural Development and Empowerment Project (PADEP) under the Ministry of Agriculture, Food Security and Cooperatives (MAFC) and Ministry of Agriculture. Ms. Swai holds a Master of Economics from the University of New England in Australia and a Post Graduate in Agricultural Economics from the University of New England in Australia.

FCS management and staff welcome the appointment of the new board members and are banking on their experience to steer FCS towards achieving its vision of an empowered, resilient, and responsible citizen realising social and economic justice and improved quality of life.

**7 Madai Crescent, Ada Estate, Plot No. 154 P.O. Box 7192 Dar es Salaam, Tanzania**
**Phone: +255-22-2664890-2 | Fax: +255-22-2664893Email: information@thefoundation.or.tz |**
**Website: www.thefoundation.or.tz Twitter: @FCSTZ | Facebook: FCSTZ**
**Youtube: Foundation for Civil Society**

# Chongolo atoa siku saba wizara kulipa fidia

**Na Mary Geofrey,**
MVOMERO

WIZARA ya Malisili na Utalii, imepewa siku saba kufika na kufanya uhakiki wa fidia kwa wananchi wa Kijiji cha Melela, Mvomero mkoani Morogoro, ambao mashamba 2,005 yaliyovamiwa na tembo na kusababisha watu 30 wa tarafa saba kupoteza maisha.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wananchi wa kijiji hicho katika ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani, uhai wa chama, kusikiliza na kututua kero za wananchi.

"Changamoto haijibiwi kwa maneno mengi. Kama tembo walivamia maeneo ya watu, Waziri ya Maliasili na Utalii, (Pindi Chana) au watendaji wa wizara na kuna mamlaka zake zilizopewa majukumu ndani ya siku saba wafike hapa kuzungumza na wananchi," alisema Chongolo.

Alisema serikali imetoa dhamana kwa watendaji kufuatilia mambo mbalimbali hivyo wana wajibu wa kupeleka majibu kwa wananchi.

"Tembo wamekula mazao watu walipwe fidia. Kinachotakiwa fedha ilipwe kwa walioharibiwa mashamba yao. Waje hapa wakae na nyie mpate haki yenu," alisisitiza Chongolo.

Awali, Mbunge wa Mvomero, Jonas Van Zeelane, aliwasilisha kero ya wananchi ambao mashamba yao yaliharibiwa vibaya na tembo hao.

Alisema katika kijiji hicho tembo wamezidi kuliko idadi ya walio hifadhini hali inayoleta usumbufu mkubwa kwa wananchi hao na kwamba wanakula mazao ya wakulima na kusababisha harasa kubwa huku hadi sasa hakuna fidia.

Katika hatua nyingine, Chongolo aliwaahidi wananchi wa wilaya ya Kilosa katika vijiji 68 visivyokuwa na huduma ya umeme kuwa watafikiwa kabla ya Aprili, mwaka huu.

Aliwaahidi kuwa Aprili ataongozana na Waziri Nishati, January Makamba, kuwasha umeme katika vijiji vyote vya wilaya hiyo.

Chongolo alipokea kero hiyo kutoka kwa Katibu wa Shina namba 10 la chama hicho, Zainabu Ally wa Kijiji cha Dumila Juu, katika kata ya Dumila, Wilaya ya Kilosa.

Alimtaka Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Fadhili Chilombe, kujibu kero hiyo, ambaye alisema kuwapo kwa gharama hizo kulitokana na kutokuwapo na mawasiliano sahihi huko nyuma.

"Kulikuwa kuna tatizo la mawasiliano ndio sababu ya kutozwa kiasi hicho, lakini kuanzia sasa watatozwa Sh. 27,000 badala ya 310,000," alisema.

Katika hatua nyingine, Chongolo alisema chama hicho kitaendea kuhoji, kukagua miradi na kusikiliza kero za wananchi kwa sababu ni jukumu lao.

"Tutahoji mpaka kieleweke, tutaendelea kuhoji na watendaji ambao wataonekana hawatufai tutachukua hatua," alisisitiza Chongolo.

Alitolea mfano wa jukumu la chama hicho, kama mmiliki wa duka ambaye ana wajibu wa kuhoji mapato, matumizi na uhalali wa shughuli zote zinazofanywa na wauzaji.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (wa pili kulia), akizungumza na wakulima wa miwa katika kijiji cha Sanje, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro jana, ambao walilalamikia kupunjwa kiwango cha utamu wa sukari wanayopeleka kiwandani kwa ajili ya kutengeneza sukari. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Mo Dewji aongeza ajira hadi 35,000

## ●Apanda kwa nafasi mbili orodha mabilionea Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo', ameongeza ajira kwenye miradi yake ya uwekezaji kutoka 28,000 hadi 35,000 kwa sasa.

Vilevile, Mo Dewji amepanda kwa nafasi mbili kwenye orodha ya mabilionea barani Afrika kutoka nafasi ya 15 mwaka jana hadi ya 13 mwaka huu, akiwa na utajiri unaofikia dola za Marekani bilioni 1.5.

Mo Dewji ni miongoni mwa waajiri wakubwa si tu kwa Tanzania, bali barani Afrika kwenye Sekta ya Viwanda.

Orodha mpya ya mabilionea duniani iliyotolewa juzi na Jarida maarufu la biashara duniani la Forbes, inamtaja Mo Dewji kama bilionea pekee kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki aliyepenya kwenye orodha mpya ya mabilionea 19 wa Afrika.

Bilionea huyo kijana ambaye mbali na biashara, amewekeza kwenye michezo, ni Mkurugenzi Mtendaji wa MeTL Group na Mwasisi wa Taasisi ya Mo Dewji ambayo inatoa huduma za hisani ikiwamo katika sekta za elimu na afya.

Hivi karibuni, Mo Dewji kupitia taasisi yake, alitoa msaada wa Sh. milioni 100 ili kusaidia matibabu ya watoto wanaougua saratani kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Jarida la Forbes limebainisha kupungua kwa utajiri wa mabilionea wa Afrika kwa dola za Marekani bilioni 3.1 katika miezi 12 iliyopita.

Forbes wamebainisha kuwa mabilionea hao 19 wanakadiriwa kuwa na utajiri unaofikia jumla ya dola za Marekani bilioni 81.5, utajiri ukiwa umepungua kutoka dola bilioni 84.9 mwaka mmoja uliopita, licha ya sasa kuwapo ongezeko la bilionea mmoja kwenye orodha mpya barani.

Kwa mujibu wa Forbes, kupungua huko kwa asilimia nne kumetokana na kushuka kwa bei ya hisa kwenye masoko mbalimbali barani Afrika.

Bilionea kutoka Nigeria, Aliko Dangote, ambaye utajiri wake umepungua kwa dola za Marekani milioni 400 kufikia dola bilioni 13.5, anaendelea kuongoza kwa utajiri barani kwa mwaka wa 12 mfululizo.

Mbali na Dangote, orodha kamili ya mabilionea barani Afrika na utajiri wao kwenye mabano, pia inawajumuisha: Johann Rupert & family (dola bilioni 10.7); Nicky Oppenheimer & family (dola bilioni 8.4); Abdulsamad Rabiu (dola bilioni 7.6); na Nassef Sawiris (dola bilioni 7.3).

Wengine ni: Mike Adenuga (dola bilioni 6.3); Issad Rebrab & family (dola bilioni 4.6); Naguib Sawiris (dola bilioni 3.3); Patrice Motsepe (dola bilioni 3.2); Mohamed Mansour (dola bilioni 2.9); Koos Bekker (dola bilioni 2.6); na Strive Masiyiwa (dola bilioni 1.9).

Pia wamo Aziz Akhannouch & family (dola bilioni 1.5); Mohammed Dewji (dola bilioni 1.5); Youssef Mansour (dola bilioni 1.5); Othman Benjelloun & family (dola bilioni 1.3); Michiel Le Roux (dola bilioni 1.2); Yasseen Mansour (dola bilioni 1.1) na Christoffel Wiese (dola bilioni 1.1).

# Jaji Kiongozi akemea rushwa utoaji haki

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani, amewataka watumishi wa mahakama kutoa haki ili kuwajengea imani wananchi, hivyo kuondoa dhana iliyojengeka kwamba hakuna huduma inatolewa mahakamani bila kutoa rushwa.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya ya Manyoni, Jaji Kiongozi alisema watumishi wa mahakama wanatakiwa kuwa mabalozi wazuri wa haki kwa kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Watumishi wa mahakama tunao uwezo wa kubadili fikra hizo kutoka kwenye kutokuaminiwa kwenda kwenye kuaminiwa kwa kufanya kazi kwa bidii na kwa haki lakini bila kufanya hivyo tutazidi kunyooshewa vidole kuwa hatutendi haki," alisema.

Jaji Siyani alisema watumishi wa mahakama wanatakiwa kujivunia na kujisifu kwa kutoa huduma bora kila mmoja kwa nafasi yake na sio kujisifu kwa vitu vingine kama majengo mazuri na mengineyo.

"Huduma bora ni pamoja na kuhakikisha miundombinu inaboreshwa ndio maana serikali imeliona hili na tunazindua mahakama zenye miundombinu miizuri kabisa," alisema.

Alisema serikali imeamua kuboresha upatikanaji wa huduma za mahakama karibu sana na wananchi ili kuondoa changamoto ya wananchi kufuata huduma hii kwa umbali mrefu sana kutoka katika maeneo wanayoishi.

"Huduma zote muhimu za kisheria zitapatikana katika majengo yetu haya ya Mahakama kama vile polisi na ustawi wa jamii ili kuepusha usumbufu wa huduma za mahakama," alisisitiza.

Jaji Siyani alisema kwa zama hizi tunapaswa kutambua umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwani hakuna huduma bora kwa zama hizi bila matumizi ya teknolojia.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema pamoja na kuboresha majengo ni muhimu hatua hiyo ikaenda pamoja na kuboresha huduma.

Alisema suala la kuchelewesha kesi bado miongoni mwa changamoto hivyo ni vyema kuhakikisha haki inatolewa kwa wakati badala ya kuchukua muda mrefu.

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## MFUMO WA KODI WA KIELEKTRONIKI KWA AJILI YA KUWASILISHA RITANI PAMOJA NA MODULI NYINGINE

**1.0 Utangulizi**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwafahamisha walipakodi na umma kwa ujumla kuwa imefanya maboresho makubwa katika mifumo yake ikigusa mifumo laini (Software) na miundombinu ya kuwezesha utendaji wa mifumo hiyo. Hatua hii inakuja katika mazingira ambayo hali ya teknolojia iliyopo haikidhi mahitaji makubwa ya walipakodi na hivyo kupelekea changamoto kwenye upatikanaji wa huduma za kimtandao hasa wakati wa tarehe za mwisho za kuwasilisha ritani, na kufanya malipo ya kodi.

Utatuzi wa changamoto hii ya mifumo daima imekuwa ni moja ya vipaumbele vikubwa vya Mamlaka ya Mapato. Mamlaka imekuwa ikifanya jitihada za dhati ili kuboresha hali ya mifumo hasa katika eneo la upatikanaji na kasi ya ufanyaji kazi. Mpango huo wa maboresho umehusisha uwekezaji mkubwa katika ununuzi na ujenzi wa mifumo laini na miundombinu muhimu ya mifumo. Miongoni mwa mabadiliko muhimu ni ukamilishaji wa kanzidata inayopatikana muda wote (High Availability Data Center - HADC) kwa lengo la kuhakikisha kuwa mifumo inapatikana na kufanya kazi kwa ufanisi wakati wote.

Juhudi za kuboresha mifumo yetu zinaongozwa na dira yetu ya kuwa "Taasisi ya mapato inayoaminika kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi" ambayo inalenga kuboresha uwezo wa taasisi kukusanya mapato zaidi kwa maendeleo ya kiuchumi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Maboresho haya kwa ujumla yanaenda sambamba na dhamira yetu inayosema "Tunarahisisha na Kuimarisha Ulipaji wa Kodi wa Hiari kwa Maendeleo Endelevu". Vilevile maboresho haya ni endelevu na yatahusisha maoni na mapendekezo ya walipakodi na wadau wengine.

**2.0 Tarehe ya kuanza kutumika kwa Mifumo ya Kodi wa Kielekroniki Iliyoboreshwa** TRA itaendelea na maboresho ya mara kwa mara na kuanza matumizi ya mifumo iliyoboreshwa kadiri inapokuwa tayari kwa matumizi. Katika awamu hii, mifumo iliyoboreshwa itaanza kutumiwa na walipakodi wote kuanzia wiki ya pili ya Februari 2023.

**3.0 Moduli za Mifumo kwa Toleo la Februari 2023**

Moduli za mifumo zilizoboreshwa na zitakazoanza kutumika mnamo Februari 2023 ni:

i) Lango la Huduma kwa Mlipakodi (Taxpayer Portal) ambayo ni lango la huduma zote za kielektroniki za TRA

ii) Moduli ya uwasilishaji wa ritani kwa njia ya kielektroniki (E-Filing) kwa kodi zifuatazo:
   - Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)
   - Kodi ya Zuio kwa Mapato ya Wafanyakazi (PAYE)
   - Tozo ya Kuendeleza Ufundi Stadi (SDL)
   - Taarifa ya Makadirio ya Kodi ya mapato inayolipwa kwa awamu (SETPI)
   - Ritani ya Kodi ya Mapato (ROI)

iii) Moduli ya Usimamizi wa kodi ya zuio (Withholding Tax Module),

iv) Moduli ya kurekebisha risiti zilizokosewa (EFD Error Management Module)

v) Mfumo wa Usajili wa Mlipakodi yaani Nambari ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) na Nambari ya Usajili wa VAT (VRN),

iv) Moduli wa Usajili wa Malipo ya Kodi (Revenue System).

**4.0 Mafunzo na Uhamasishaji kwa Umma**

TRA imeandaa na kuanza utekelezaji wa program ya uhamasishaji na mafunzo juu ya mifumo iliyoboreshwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile semina za ana kwa ana, warsha, mafunzo ya mtandaoni, vipindi vya Televisheni na Redio. Lengo la programu hii ni kuwafikia walipakodi na wadau wote ndani ya muda mfupi na kuwapatia ujuzi na uwezo unaohitajika katika kutumia mifumo iliyoboreshwa kwa ufanisi. Hivyo basi, TRA inawataka walipakodi wote na wananchi kwa ujumla kufuatilia na kushiriki mafunzo hayo ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Taarifa juu ya mafunzo zitatolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo, redio, televisheni, magazeti, tovuti na akaunti za mitandao ya kijamii za TRA.

**5.0 Wajibu wa Walipakodi na Umma kwa Ujumla**

Mamlaka inatambua umuhimu wa walipakodi na umma kwa ujumla katika kila jambo inalofanya. Mamlaka inategemea sana maoni na ushauri toka kwa walipakodi na umma kwa ujumla katika kipindi cha mpito kuelekea matumizi ya mifumo iliyoboreshwa na katika mchakato mzima wa maboresho ya mifumo katika siku za usoni. Hii inatokana na ukweli kwamba walipakodi na umma kwa ujumla ndio watumiaji wakubwa wa mifumo hiyo. Kwa minajili hiyo, Mamlaka inapenda kuwaalika walipakodi wote na wadau kutoa maoni na ushauri kwa lengo la kujenga mifumo iliyo bora na ya kisasa zaidi.

**6.0 Hitimisho**

TRA inapenda kutoa shukurani zake za dhati kwa walipakodi na umma kwa ujumla kwa kuendelea kujitoa katika kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni na taratibu za kodi kwa hiyari hasa uwasilishaji wa ritani na ulipaji wa kodi kwa njia ya mtandao katika kipindi chote ambacho mifumo iliyopo imekuwa na changamoto ya upatikanaji na kasi ya ufanyaji kazi.

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Kidatah

A. J. Kidata

**Kamishna Mkuu**

21725701

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utaratibu viongozi kusikiliza kero za wananchi unasaidia kuibua madudu

**KUNA** baadhi ya viongozi ambao wamejiwekea utaratibu wa kukutana na wananchi ili kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Katika utaratibu huo viongozi wengine huwakaribisha wananchi ofisini kwao na mmoja mmoja huingia na kueleza kero au mapendekezo yatakayowarahisishia kuongoza vizuri.

Baadhi yao huamua kufanya ziara kwa kuwatembelea wananchi walipo na kufanya mikutano ya hadhara na hapo hupewa nafasi ya kuuliza maswali au kutaja kero zinazowakabili.

Ziara hizo za viongozi huibua madudu mengi ambayo yalikuwa yamejificha kwa wale wanayoyafanya kujiamulia vyovyote wakijua hakuna anayewafuatilia.

Moja ya madudu yaliyoibuliwa katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alipotembelea Wilaya ya Manyoni na kuwataka wananchi waeleze kero zao na ndipo aliposimama mwananchi mmoja na kulalamika kuwa baadhi ya madaktari wanakwenda kazini wakiwa wamelewa hali inayowatia hofu kwa usalama wa maisha yao.

Mwananchi huyo alilalamika kuwa alimpeleka mwanawe hospitali na kumkuta daktari akiwa amelewa chakali na kushindwa kuwahudumia.

Hali hiyo ya baadhi ya madaktari kufika kazini wakiwa wamekunywa pombe imedaiwa kujitokeza mara kwa mara katika hospitali yao na wananchi kuingiwa hofu ya usalama wa maisha yao.

Kwa kweli hiyo inatia hofu kwa sababu daktari anategemewa katika kumsaidia mgonjwa kujua tatizo lake na kumwandikia dawa ili aweze kupata tiba.

Kama daktari huyo anayetegemewa anafika kazini akiwa hajiwezi kwa kulewa na wagonjwa wakisubiri huduma yake hilo ni tatizo kubwa na halina budi kuchukuliwa hatua za haraka ili wananchi wasaidiwe kuondokana na kero hiyo.

Tabia ya baadhi ya watumishi kuingia kazini wakiwa wamekunywa pombe inapunguza ufanisi wa kazi na vilevile inahatarisha maisha, ustawi wa taasisi au kampuni anayofanyia kazi.

Miongoni mwa watu hao wanaaminiwa na viongozi wao kwa kupewa nafasi za juu, lakini wanashindwa kuonesha ufanisi na kuwaangusha wale waliowapendekeza kushika nafasi hizo.

Mara nyingi watu wa aina hiyo wanapokwenda kutafuta kazi wanakwenda kwa unyenyekevu, lakini wanapozipata wanasahau shida walizopitia na kuanza kuchezea nafasi walizozipata kwa kuingia kazini wakiwa wamechelewa huku wakiwa wamekunywa pombe.

Wengine hudiriki kuondoka kazini huku wakiwa na majukumu mezani mwao ya kufanya na kuchelewesha mipango mingine na kwenda kwenye shughuli nyingine zisizo za kiofisi.


Watu hao huwa wa kwanza kulalamika inapotokea kampuni au taasisi kutikisika kiuchumi na kuamua kupunguza wafanyakazi, akiwa kwenye orodha ya wanaotakiwa kuondoka.

Anasahau kuwa alipokuwa kazini alikuwa akifanya mambo ya ovyo na kutothamini kampuni yake inayomlipa mshahara kila mwezi ambao pengine alikuwa akiwazidi hata wenzake wanaofanyakazi kwa ufanisi na nidhamu.

Ndiyo maana kwa wale waliobahatika kutembelea nchi za wenzetu walioendelea, watu wanalipwa kutokana na kazi wanazofanya. Wengine hudiriki kufanya kazi zaidi ya moja ili aweze kupata kipato zaidi cha kumsaidia kuendesha maisha yake vizuri.

Wewe unayefanyakazi kwa kulipwa mshahara kila mwezi ambao haulingani na kazi unazozifanya ni sawa na kumwibia mwajiri wako kwa kuchukua malipo ambayo hukuyafanyia kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# CHADEMA mwendo wa 'No Hate No Fear'

**CHADEMA** imezindua mikutano ya hadhara katika viwanja vya Furahisha jijini Mwanza wiki chache zilizopita inaendelea na mikutano hiyo kwenye mikoa mingine ukiwamo uliofanyika jijini Dar es Salaam na kuhutubiwa na Makamu Mwenyekiti Tundu Lissu, aliporejea akitokea uhamishoni nchini Ubelgiji.

Tofauti na matarajio ya baadhi ya wanachama wa chama hicho kuwa huenda viongozi hao 'wangeshambulia' serikali kwa maneno, katika hotuba zaa lakini wakahimiza umuhimu wa maridhiano.

Kwa mfano, Mwenyekiti Freeman Mbowe, anakumbushia kaulimbiu ya chama ya 'No Hate No Fear' kwamba ni vyema izingatiwe, kwa kuwa inalenga kujenga demokrasia, utengamano, uhuru, ustawi wa taifa lenye furaha na maendeleo kwa umoja.

Akawaambia pia viongozi, makada na wanachama wa vyama vyote vya siasa, kuwa taifa haliwezi kuongozwa kwa misingi ya visasi na kugawa watu kwa sababu ya tofauti zao za itikadi za vyama.

Pamoja na kwamba zimekuwapo na kauli mbalimbali kutoka hata ndani ya chama kuhusu Mbowe, kuwa huenda 'amelambishwa asali' hadi anaamua kulainika na kutofanya siasa za uanaharakati, ninadhani yuko sahihi.

Kwa sababu ni kweli kwamba, taifa haliwezi kuongozwa kwa misingi ya visasi na kugawa watu kwa kufuata tofauti zao za itikadi za vyama au 'kushambuliana' kwa maneno majukwaani.

Jambo la msingi ni kutafuta maridhiano kama ambavyo kiongozi huyo alifanya na sasa matunda yake yameonekana, kufuatia kuruhusiwa kwa mikutano ya vyama vya siasa iliyozuiwa kwa zaidi ya miaka sita.

Ingawa inaweza kuonekana ni vigumu, lakini ninadhani uamuzi wa Mbowe wa kumshukuru Rais Samia Hassan, kwa jinsi alivyoruhusu maridhiano yaliyozaa matunda ya kuwapo kwa mikutano ya hadhara, ni uungwana.

Ninaona hatua ya viongozi wa CHADEMA kujikita kwenye hoja zaidi badala ya kushambulia watawala, kama jambo la msingi, na ni vyema wanachama wao wakaichukulia kama njia bora ya kusimamia maridhiano.

Chama kinaamini katika 'no hate no fear', kwa lengo la kujenga taifa lenye furaha, demokrasia, uhuru, utengamano, ustawi na maendeleo ya watu bila kujali tofauti za aina yoyote, hivyo kaulimbiu hiyo ingeachwa ifanye kazi.

Ninaamini kupitia kaulimbiu hiyo, viongozi wa chama wanaweza kuendelea na mikutano yao ya hadhara kwa kujenga hoja zenye mashiko bila woga na pia bila kutukana au 'kushambulia' serikali kwa maneno.

Lakini siamini kuwa mtu anapoachana na siasa zisizo na tija, ni kulambishwa asili, hatua hiyo ni sawa na kuepusha siasa zisizo na tija zinazoweza kuwamsha chuki miongoni mwao.

Kimsingi, siasa hazitakiwi kuwa za kutukanana au kudhalilishana majukwaani, lakini kutowashambulia viongozi wa serikali kwa maneno haimaanishi kuwa upinzani hauwezi kuwakosoa na kuwaambia ukweli.

Kama sikosei, kaulimbiu ya 'No hate no fear' inagusa pia kusamehe ya nyuma na kusonga mbele bila woga, hivyo kuendeleza maneno kuwa kuna ulambishwaji wa asali, ni sawa na kuwakatisha tamaa viongozi wa chama.

Ikumbukwe kuwa, tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani Machi 2021 kumekuwapo na mabadiliko kadhaa ya kimtazamo yanayoonekana katika siasa, vyama vya siasa, wanasiasa na demokrasia kwa ujumla.

Amekutana na wanasiasa wa upinzani, akaruhusu maoni ya kuboresha kanuni za mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, uhuru wa vyombo vya habari wa kukosoa na mengine mengi katika anga za siasa na demokrasia.

Lakini akaunda kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, chini ya uenyekiti wa Prof. Rwekaza Mukandala na kumwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge kuandaa kanuni zinazoelekeza jinsi ya kufanya mikutano ya hadhara.

Hivyo, wanatuhumu viongozi wao kuwa wamelambishwa asali, wangeiona pia nia njema ya Rais kwa vyama vya upinzani, ambayo ni kutaka siasa za ushindani wa hoja na si matusi au 'kushambuliana' kwa maneno.

TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

# Nuru kumaliza tatizo maji Dar yang'ara

**Na Joseph Mwendapole**

MWANGA wa kumaliza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani umeanza kuonekana kutokana na ujenzi wa Bwawa la Maji Kidunda mkoani Morogoro, utakaogharimu Sh. bilioni 346, kuanza hivi karibuni.

Mradi huo unatekelezwa na serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), baada ya kuanza kutekelezwa, unatarajiwa kukamilika mwaka 2026.

Akizungumza hivi karibuni katika kikao kazi kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa, Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu.

Luhemeja alisema baada ya kukamilika, mradi utakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 190 na utakuwa suluhu ya upungufu wa maji Dar es Salaam na mkoa wa Pwani.

"Tumekuja kuomba ushirikiano na uongozi wa mkoa katika usimamizi wa mradi huu ikiwa ni pamoja ulinzi wa watu na miundombinu ambayo itawekwa," alisema Mhandisi Luhemeja.

Alisema mradi huu wa kimkakati utahitaji ulinzi wa miundombinu yake ili utekelezwe ndani ya muda uliokusudiwa.

Mhandisi Luhemeja alisema shughuli mbalimbali zimekwishafanyika kuelekea utekelezaji wa mradi huo ikiwamo ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi na ujenzi wa huduma muhimu za kijamii kama vile shule na kituo cha afya.

Shughuli zingine, kwa mujibu wa Luhemeja, ni ujenzi wa miundombinu ya barabara na upimaji wa viwanja 1,000 katika makazi mapya.

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Musa Ali Musa, aliishukuru DAWASA kwa kutambulisha mradi rasmi kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na kutoa rai kwa mamlaka kuongeza nguvu zaidi katika ulinzi wa vyanzo vya maji ambavyo vitasaidia upatikanaji wa maji ya kutosha kwenye utekelezaji wa mradi huo.

"Nitoe rai kwa DAWASA kushirikiana na wadau ikiwamo Bonde la Wami Ruvu katika kuendelea kusimamia ipasavyo vyanzo vya maji ambavyo ni tegemeo kubwa la wananchi wa Dar es Salaam na Pwani," alisema. Alisema Mto Ruvu unahudumia zaidi ya asilimia 76 ya wateja wa DAWASA, hivyo bila kuimarisha usimamizi thabiti hawatafikia malengo yanayotarajiwa.

Mwassa kwa upande wake alielezea kufurahishwa na hatua ya serikali kuupa hadhi mkoa wa Morogoro na kuwa ni hazina ya maji, umeme na chakula, hivyo italeta maendeleo makubwa katika mkoa.

"Tunaishukuru serikali kwa kuendelea kuleta maendeleo katika mkoa wa Morogoro. Tunajipanga kutumia fursa zilizoko. Sasa mkoa wetu unajipambanua kama kitovu cha huduma za maji na umeme na kupitia mradi huu wananchi watanufaika zaidi na huu mradi kijamii na kiuchumi," alisema.

"Kazi kubwa inayoendelea mbele yetu kwa sasa ni kutatua changamoto ya mifugo katika vyanzo vya maji na kuondoa wavamizi ikiwa ni katika kusimamia sheria zilizoko na maelekezo ya viongozi," aliongeza.

Mwassa alisema kazi hii ni endelevu na itasaidia kutoa uhakika wa ulinzi wa vyanzo vya maji ambavyo vina faida lukuki kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Mkuu huyo wa Mkoa aliitaka DAWASA kutenga eneo la kujenga ofisi maalum kwa ajili ya kuwezesha taasisi za ulinzi kufanya kazi kuanzia katika kipindi cha ujenzi na hata baada ya mradi wa Kidunda kukamilika.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Kampuni ya Heritage Insurance, Thecla Magashi (kulia), akimtunuku zawadi wakala wa Profound Insurance Agency, Marynice Pallangyo, jijini Dar es Salaam juzi, kutokana na utendaji kazi bora kwa 2022 na jukumu muhimu la kutoa huduma za bima kwa wateja wa kampuni hiyo nchini kote. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Heritage Tanzania, Manasseh Kawoloka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanawake watoa neno wanaume kuwapo kwenye mpango kazi taifa

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi, wameomba kuondolewa kwa wanaume katika rasimu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili kwa Wanawake na Watoto wa mwaka 2023-2027.

Wakizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, wanawake viongozi wa mtandao huo, walisema katika vikao vyote walivyoshirikishwa vya kujadili mpango huo, waliokuwapo kwenye mpango ni wanawake na watoto lakini cha kushangaza wanaume wameingizwa ghafla.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebecca Gyumi, alisema ni vyema maoni ya wadau yakaheshimiwa kwa kuacha mpango huo kuendelea kuwatambua wanawake na watoto kama kundi linaloathirika zaidi na ukatili wa kijinsia.

"Wanaume waendelee kuripoti vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi yao kwa kutumia mifumo mingine ya kisheria bila kuingilia jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika kuwakomboa wanawake na watoto ambao ndio waathirika wakubwa,"alisema.

Mratibu wa Kitaifa wa Ulingo, Dk. Avemaria Semakafu, alisema walishiriki katika vikao vyote vya wadau ikiwamo rasimu ya kwanza, ya pili na ya tatu ya mpango huo, lakini kundi la wanaume halikuwapo.

"Kwa hiyo tunashangaa hiyo ya mwisho ya kwenda baraza la mawaziri, mwanaume ameingizwa, katokea wapi?"alihoji Dk. Semakafu.

"Tunatoka nje ya mstari ya kile tulichokusudia, lakini maoni ya wadau hayakusema kwamba wanaume ni kipaumbele katika mpango huo. Tukiwa kama wadau sisi ndio wahusika, ndio jamii, unapotaka kutengeneza kitu unaangalia ni kwa nini unafanya hivyo hatutengenezi tu lelemama," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, alisema hakuna utafiti wowote uliofanywa kwa kina na kutoa idadi ya kutosha ya wanaume ambao wamefanyiwa unyanyasaji au ukatili ili kutosha kuridhisha kuwekwa kwenye mpango huo.

"Huu ni mwendelezo wa mkakati uliokuwapo wa wanawake na watoto, ni vema kunapotokea jambo la kuongezwa iwapo na sababu ya msingi badala ya kuongezwa kiholela, huu ni mpango wa kitaifa ambao unaenda kuweka sharti katika mipango ya Bara la Afrika na dunia. Kwa maana hiyo Tanzania tutakosa namna ya kuweka michango yetu ya hali halisi ya ukatili wa kijinsia katika nchi endepo tunaanzisha jambo jipya katikati ya njia," alisema.

Mary Ndaro, mwanaharakati wa kupigania haki za wanawake na watoto, alisema pamoja na kwamba wapo baadhi ya wanaume wanaopitia ukatili, lakini bado namba yao ni ndogo ukilinganisha na ile ya wanawake na watoto.

"Na hata serikali ilikuja na mpango huu wa kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa sababu ndio waathirika wakubwa," alisema.

## Wapatiwa msaada Wiki ya Sheria Dar

**Na Frank Monyo**

WATU 175 wamepatiwa huduma ya msaada wa kisheria na Shirika la Legal Services Facility (LSF) wakiwamo wanaume 73 na wanawake 102 katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Aidha, taasisi hiyo imeshughulikia mashauri mbalimbali yakiwamo migogoro ya ndoa, matunzo ya watoto, mirathi na migogoro ya ardhi.

Akizungumza wakati wa kufunga maadhimisho hayo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema wanashirikiana na mahakama kama chombo cha kutoa haki kwa ajili ya kukuza upatikanaji wa haki Tanzania kwa kuwasaidia wananchi kupata haki zao kwa ajili ya maendeleo.

"Wiki ya Sheria imekuwa muhimu kwetu kama wadau wa mahakama kwani kupitia wasaidizi wa kisheria tumeweza kutoa huduma bure kwa wananchi waliotembelea banda letu kwa njia ya usuluhishi. Kupitia wiki hii tumesaidia watu 175 ambapo wanaume ni 73 na wanawake 102," alisema Ng'wanakilala.

Alisema LSF kupitia wasaidizi wa kisheria jijini Dar es Salaam inashughulikia mashauri mbalimbali, yakiwamo migogoro ya ndoa, matunzo ya watoto, mirathi pamoja na migogoro ya ardhi.

Naye Msuluhishi kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Usuluhishi, Jaji Dk. Zainab Diwa Mango, alisema mahakama sasa zinakabiliwa na mashauri mengi yanayoendelea, ambayo pia yanahitaji ushahidi, ili kufanya uamuzi wa mwisho, jambo ambalo hulazimika kuchukua muda mrefu tofauti na kutumia njia ya usuluhishi.

"Usuluhishi hauchukui muda mrefu, unachukua muda wa siku 30 tu. Hii ni kwa mujibu wa katiba yetu Ibara ya 107A(1) (d), ambayo inasisitiza kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika mgogoro," alisema Dk. Mango.

Alibainisha kuwa usuluhishi unapunguza muda mwingi mahakamani na kumpa muda mteja muda wa kufanya shughuli za kiuchumi, kwa kuwa katika usuluhishi hakuna dhana ya kila mtu kutaka kushinda, kitu ambacho huleta changamoto kubwa kwenye mashauri yanayoendeshwa mahakamani.

"Kituo chetu cha usuluhishi kilianza mwaka 2015 na mwaka huu tumetoa taarifa maalum ya utekelezaji wa shughuli zetu kwa kipindi cha miaka saba. Kupitia kauli mbiu ya mwaka huu itasaidia kuonesha umuhimu wa usuluhishi kwa wananchi," alisema Dk. Mango.

Mmoja wa wanufaika wa huduma hizo, Joyce Massawe, alisema alikuwa na mgogoro wa mtoto kati yake na ndugu wa marehemu mume wake ambao walimnyang'anya bila kufuata utaratibu lakini maadhimisho ya Wiki ya Sheria yamesaidia kupata suluhu nzuri kati yake na ndugu hao baada ya kuitwa ili kufanya usuluhishi.





## LSF, NSC wazindua mradi kuwawezesha wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la LSF kwa kushirikiana na Taasisi ya North-South Cooperation kutoka Luxembourg wamezindua mradi wa miaka miwili utakaotambulika kama 'wanawake tunaweza'.

Mradi huo utakaotekelezwa wilayani Longido mkoani Arusha kwa ajili ya uwezeshaji wa wanawake na jamii ya Kimasai nchini katika nyanja ya kiuchumi na kijamii.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huu jijini Arusha, Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema LSF imeamua kutekeleza mradi huo kwa kushirikiana na wadau wengine ili kusaidia jamii ya kimasai hususani wanawake na watoto wa kike, ambao wamekuwa nyuma katika hatua za maamuzi, umiliki wa rasilimali ikiwamo ardhi na mifugo, pamoja na fursa sawa ya kwenda shule.

Alisema mradi huo unalenga kuwezesha kiuchumi wanawake wa Kimasai kwa kuwasaidia kuunda vikundi vya kiuchumi, kuwajengea uwezo katika masuala ya kibiashara na ujasiriamali, pamoja na kuwawezesha kupata soko la bidhaa mbalimbali watakazozizalisha.

Lulu alisema katika kuhakikisha kuwa jamii hususani wanawake na watoto wa kike wanawezeshwa, mradi huo utakwenda pia kusaidia kuboresha upatikanaji wa elimu kwa watoto wa kike kwa kuwajengea mabweni, kuunda klabu za wasichana shuleni, pamoja na utoaji wa taulo za kike shuleni kutoka katika vikundi vya wanawake vitakavyozalisha bidhaa hizo.

"Jamii ya Kimasai ni ya kipekee nchini Tanzania kutokana na udumishaji wa mila na desturi zake kwa kipindi kirefu. Uchumi wa jamii ya kimasai unategemea zaidi shughuli za ufugaji kwa asilimia 85 ya shughuli zote za kiuchumi zinazoendeshwa na jamii hii.

Njia kuu za uchumi pamoja na uzalishaji mali kwa jamii ya kimasai zinamilikiwa na kuendeshwa na wanaume, hali inayosababisha haki za wanawake na wasichana wa kimasai kukiukwa," alisema.

Alisema kuanzishwa mradi huo wilayani Longido kutawezesha kutatua baadhi ya matatizo na kuwawezesha wanawake wa kimasai kijamii na kiuchumi.

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido, Hassan Ngoma, aliwapongeza LSF pamoja na wadau wa maendeleo kutoka Luxemburg kwa kuona vyema na kuamua kushirikiana kutekeleza mradi huu.

Ngoma, alisema ujenzi wa mabweni ya watoto wa kike katika shule za sekondari za Lekule na Namanga utawezesha kutatua matatizo ya watoto kubanana kwenye bweni moja na kuongeza idadi ya watoto shuleni na kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu utakaochochea ufaulu wa wanafunzi kuongezeka.

Aidha, alisisitiza pia kutawaongezea nguvu ya kupambana na shughuli za uzalishaji utakaowawezesha kuwainua kiuchumi, kutoa huduma bora na malezi kwa wototo na kukuza ustawi wa jamii nzima kwa ujumla.

# Aliyefariki kwa kupigwa na wazazi wake azikwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANAFUNZI wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Elerai iliyoko Arusha, Shadya Ibrahimu (13) aliyefariki kwa kupigwa na baba yake mzazi, Ibrahimu Omari kwa madai ya kuchelewa kununua mchicha wa Sh.300 amezikwa jana Olematejoo 'A' Kata ya Sakina.

Akizungumza na waandishi wa habari mama mdogo wa marehemu, Zakhia Hussein, alisema marehemu alikuwa na tabia ya kumtembelea kwake mara kwa mara na kulalamika juu ya mama yao wa kambo kutowapa chakula.

"Shadya amekuwa akiniambia mama yao huyo anawanyima chakula na wakati mwingine alikuwa akiachiwa fedha na baba yao awanunulie chakula anaenda kuwanunulia mihogo," alisema.

Alisema hali hiyo alipokuwa ikiendelea alilazimika kumfuata mwanamke huyo na kugombana naye juu ya hilo.

"Kweli nimesikitika sana na habari hii niliipata na nawaomba wanawake wenzangu mkiona mtoto amekosa jengeni tabia ya kuwaonya wenyewe na kwa adhabu inayostahili na inayoendana na umri wao na siyo kuwachongea kwa baba zao kama alivyofanya huyu," alisema. Mama mzazi wa marehemu Shadya, Rukia Hussein alishindwa kuzungumzia juu ya tukio hilo.

Naye mama mkubwa, Safiuna Rashidi alisema alipata taarifa za kifo hicho cha mtoto huyo akiwa kazini.

"Lakini nilifuatilia kwa karibu nimesikia alikuwa anampa adhabu ndogo kwa kumchapa kwa nyaya za mwavuli ambazo zisingeweza kumuua, mimi kwa amri yangu angesamehewa maana aliwapenda wanaye na aliwalea tangu wakiwa wadogo sana, ila kwa kuwa ni masuala ya serikali basi sheria iendelee,"alisema.

Shadya alifarikia dunia Januari 27, mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku huko Olematejoo 'A' Mtaa wa Sakina, jijini Arusha baada ya kuchelewa kurudi nyumbani alipotumwa kununua mchicha wa Sh.300 na mama yake wa kambo na kusababisha baba yake (Ibrahimu) kumchapa hadi mauti yalipomfika.



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Halima Bulembo (kushoto), akikabidhi nyaraka kwa Mkuu mpya wa wilaya hiyo, Juma Saidi Irando, wakati wa hafla ya makabidhiano ya ofisi, wilayani humo jana. Kulia ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Desderia Haule. Bulembo, amehamishiwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yajenga daraja la bil.3/- Mto Mkomazi

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

WANANCHI 18,000 wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, waliokuwa wakishindwa kuvuka Mto Mkomazi sasa wataondokana na adha hiyo baada ya serikali kutengeneza daraja la Sh.bilioni tatu.

Kabla ya ujenzi wa daraja hilo, wakazi hao walikuwa wakipoteza ndugu zao kwa kuliwa na mamba pindi wanapovuka.

Fedha za utekelezaji wa ujenzi wa daraja hilo zinatokana na tozo ya mafuta, ambapo mradi huo unatajwa utafungua mawasiliano ya Barabara ya Kwasunga- Mswaha.

Jana, Kaimu Meneja wa TARURA, Andrew Gewe, alisema mradi huo utakaogharimu Sh. bilioni 3.83, unatarajiwa kukamilika Septemba 9, mwaka huu.

"Mpaka sasa mradi umefikia asilimia 67 na muda ambao umeshapita ni miezi tisa, ambayo ni sawa na asilimia 53.

"Kama mnavyoona maji ya mto huu hayakauki na wananchi wa vijiji hivi walikuwa wanapata tabu katika kuvuka wakitumia mitumbwi, lakini TARURA wakafanya utaratibu wa kujenga daraja, kwa ajili ya wananchi kupita kwa miguu.

"Hata hivyo, serikali imeona kwamba kuna umuhimu wa kuweka daraja ambalo litaweza kuhudumia wananchi na maendeleo. Kwa sababu kuna kilimo cha mkonge kinaendelea pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi, hivyo serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga daraja hili," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwasunga-Mpirani, Lucas Sempoli, alisema mto huo ambao unaunganisha kata tatu za Magilagereza, Makuyuni na Mswaha Darajani, kwa miaka mingi wamekuwa wakipoteza ndugu zao, kwa kuliwa na mamba pamoja na viboko, wakati wa kuvuka mto huo.

Alisema: "Kuna wanafunzi ambao wanapata huduma ya shule, ng'ambo ya huu mto, ambao una desturi ya kujaa na kukauka. Unapokauka, watoto wanapita vizuri lakini ukijaa maji unakuwa ni hatari zaidi.

"Huko ng'ambo kuna mashamba yetu ya asili na wananchi wa kata zote tatu tunashirikiana katika mipaka.

"Kwa hiyo watu wa Mswaha-Majengo, wanashindwa kuja kwenye mashamba yao huku kwetu na mtu wa Kwasunga au Magilagereza, nao wanashindwa kwenda kule kutokana na adha ya maji kujaa kwa kuhofia kuliwa na mamba."





# Mwanamke apambana na fisi, aokoa familia yake

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKAZI wa Kijiji cha Mwamalata wilayani Kishapu, Mbuke Jishanga, amepambana na fisi aliyetaka kuwashambulia watoto wake wanne, pamoja na mifugo nyumbani.

Tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 7 usiku wakati watoto hao wakiwa wamelala kwenye nyumba nyingine tofauti na ya mama yao, ndipo wakavamiwa na fisi na kuanza kushambuliwa sehemu mbalimbali za miili yao.

Akisimulia tukio hilo, mama huyo alisema majira ya saa 7 usiku alisikia kelele kwenye nyumba ambayo wamelala watoto wake na alipotoka nje akamkuta kijana wake mmoja akishambuliwa na fisi, ndipo akashikwa na ujasiri wa kuchukua panga na kumkata mnyama huyo kichwani.

Alisema wakati akiendelea kupambana na fisi alikuwa akipiga kelele za kuomba msaada kwa majirani, ambao walifika na kumsaidia na hatimaye wakafanikiwa kumuua fisi huyo.

Watoto wake kwa sasa wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kishapu.

"Sisi Wasukuma huwa tuna desturi watoto wa kiume lazima walale karibu na zizi la mifugo ili kuwalinda dhidi ya wanyama wakali, wakati wakiwa wamelala ndipo wakavamiwa na fisi, niliposikia kelele nikatoka nje na kukuta mtoto wangu mmoja aking'atwa ikabidi nipambane naye huku nikiwa na panga mkononi,"alisema na kuongeza:

"Nilipomkata panga kichwani akajibamiza ukutani, nikamwona anajiweka sawa kwa ajili ya kunirukia na mimi nikashika panga vizuri, aliporuka tu akakutana na panga tena akaanguka chini huku nikiendelea kupiga kelele za kuomba msaada ndipo wakaja majirani wakammalizia kumuua, nikawachukua watoto wangu nikawakimbiza hospitali," alisema.

Aliwataja watoto ambao walishambuliwa kuwa ni Jishanga Izengo aliyeng'atwa sehemu ya pua, Kanizio Joseph (mapajani), Lazaro Emmanuel (kichwani na mikononi), Malambi Mayala (kichwani na shingoni).

Kijana mkubwa wa familia hiyo, Joseph Shija, ambaye hakujeruhiwa, alisema fisi huyo wanamhusisha na imani za kishirikina akisema ni maajabu kwa fisi huyo kuwafuata wao ndani ya nyumba badala ya kwenda kushambulia mifugo kwenye zizi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kishapu, Dk. Mohamed Mkumbwa, alikiri kuwapokea majeruhi hao wakiwa katika hali mbaya kutokana na majeraha waliyoyapata.




Meneja Mauzo wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) Mkoa wa Kagera, Anna Msomba (kushoto), akikabidhi cheti cha ufadhili wa masomo kupitia mpango wa Kilimo Viwanda kwa mmoja kati wa wanafunzi 24 wa Chuo cha Kilimo na Mifugo cha Igabiro, Evona Fredinarnd, wakati wa hafla chuoni hapo wilayani Muleba mkoani Kagera mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mkurugenzi wa Uhusiano wa SBL, John Wanyancha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba elimu ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele itolewe maeneo ya vijijini

**Na Vitus Audax,** MAGU

WANANCHI wilayani Magu mkoani Mwanza wameiomba serikali pamoja na wadau wa maendeleo kuweka mkazo katika utoaji wa elimu sambamba na matibabu ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele maeneo ya vijijini.

Wamesema wengi wao hawana uelewa wa magonjwa hayo ambayo baadhi yamekuwa yakisababishwa na uchafuzi wa mazingira.

Wakizungumza na Nipashe wakati wa siku ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele, baadhi ya wananchi hao walisema idadi kubwa ya wananchi vijijini hawana elimu ya kujikinga na magonjwa hayo.

"Mara ya kwanza macho yalikuwa yakiniwasha nilijua tu ni hali ya kawaida kutokana na matumizi ya kuni na mkaa lakini walivyokuja wahudumu kutoka Shirika la Ima World Health na kunipima macho nikaambiwa kuwa natakiwa kufanyiwa upasuaji kutokana na kuwa na ugonjwa wa trakoma," alisema Rahel Masanja mkazi wa Magu. Aliongeza kuwa bila kuelimishwa juu ya ugonjwa huo angepata matatizo zaidi kwa mujibu wa wataalamu hao hivyo kuiomba serikali kuweka mkazo zaidi kwani wapo wagonjwa wengine ambao bado wanatumia dawa za kienyeji ilihali ugonjwa huo unatibika kwa upasuaji. Mkazi mwingine, Alex Msumate ambaye ni Mratibu wa Shirika la Ima World Hearth alisema katika kipindi cha miaka 20 wamekuwa wakifanya kazi na Wizara ya Afya wamekuwa wakitoa dawa katika halmashauri mbali sambamba na kutoa vifaa tiba kwa ajili ya kufanya upasuaji hasa wa vikope kwa wenye ugonjwa wa trakoma.

Mratibu wa ugonjwa wa trakoma kitaifa kutoka Wizara ya Afya, Hope Rusibamayila alisema wameanza kutekeleza afua mbili ambazo ni utoaji wa kingatiba kwa ngazi ya jamii sambamba na umezeshaji wa kingatiba kwa wagonjwa pamoja na huduma za matibabu.

# Ma-DC wapya watakiwa kufanya kazi kwa weledi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, amewataka wakuu wapya wa wilaya walioteuliwa kutenda kazi kwa weledi na kuwaletea maendeleo wananchi badala ya kwenda kuimarisha makambi yasiyo na tija katika uongozi.

Alitoa kauli hiyo wakati wa hafla fupi ya kuwaapisha wakuu wapya wa Wilaya ya Chato, Nyang'hwale na Geita mkoani humo na kueleza kuwa dhumuni la wao kuteuliwa ni pamoja na kuwatumikia wananchi na kutatua matatizo yao.

Aidha, alisema ili kutunza imani ya Rais Samia Suluhu Hassan juu yao ni pamoja na kufuatilia upotevu wa mapato, fedha ya serikali pamoja na kukomesha migogoro kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

"Nendeni mkafanye kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa kutoa ushirikiano na kutekeleza majukumu ya kiserikali msimwangushe Rais,"alisema.

Alisema wakuu hao wanawajibu wa kuhakikisha wananchi wanasomewa mapato na matumizi, mikutano ya hadhara.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Geita, Niclous Kasendamila, alisema kuwa kazi ya ukuu wa wilaya ni kutumia fursa, hivyo aliwataka kumwomba Mungu ili awajalie afya njema, hekima na busara na kutenda haki katika kutekeleza majukumu yao.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Profesa Godius Kahyarara, aliwapongeza wakuu hao na kuwataka kwenda kufanya kazi kwenye maeneo yao kwa kuzingatia viapo vyao na kuitekeleza ilani ya CCM.

Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba, alisema : "Vyeo vyetu ni tofauti na wabunge, madiwani wao hufanya kampeni na kupigiwa kura sisi tunateuliwa.

**Aidha, alisema ili kutunza imani ya Rais Samia Suluhu Hassan juu yao ni pamoja na kufuatilia upotevu wa mapato, fedha ya serikali pamoja na kukomesha migogoro kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.**



Ukurasa 12

**Vita Russia, Ukraine huzuni kwa wajasiriamali kila kona**



Ukurasa 13


SMZ inakumbuka ahadi ya kurekebisha sheria kandamizi?


# siasa

JUMATANO FEBRUARI 1, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 14

MARTIN LUTHER KING JR 'NINAYO NDOTO'

**Maono yake yanavyobaki kuwa fikra inayoishi kwa wanasiasa, wanaharakati**

## CHONGOLA AONA FEDHEHA MORO

# Viongozi, watendaji waangamiza vijiji kisa? Hongo za mifugo, fedha

**Na Mary Geoffrey**, MOROGORO

KUPOKEA rushwa na zawadi kutoka kwa wafugaji ili kuwaachia wafanye wanavyopenda kwenye mashamba na makazi ya wakulima mkoani Morogoro, kumeigusa CCM na sasa Katibu Mkuu Daniel Chongolo, anaahidi kupambana na wahujumu uchumi hao.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwasa, anasema kuwapo kwa mifugo mingi kumesababisha uharibifu wa vyanzo vya maji, mapigano na mauaji, migogoro ya ardhi, watu kadhaa kupoteza maisha na kuleta athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kupungua mvua.

Anawaonya watendaji na viongozi wa vijiji wasio waadilifu, kuwa wanapokea rushwa na kuruhusu mifugo kuingia katika vijiji na makazi ya watu kinyume cha taratibu, vitendo hivyo sasa vifike mwisho.

Chongolo anayasema hayo akizungumza kwa nyakati tofauti wilayani Gairo na Mvomero mkoani Morogoro katika mwendelezo wa ziara ya siku tisa ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo, uhai wa chama, kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Akiwa ameambatana na Katibu wa NEC, Itikati na Uenezi, Sophia Mjema na Katibu wa NEC na Oganaizesheni Issa Haji Ussi, anasema Morogoro ina mifugo milioni 1.7 lakini utafiti unaonyesha ongezeko la mifugo zaidi ya 3,000.

"Hawa ng'ombe siyo ndege useme wameruka kutoka mkoa mmoja kufika mwingine, kote wanakopita hakuna watendaji, wenyeviti wa vijiji wanaruhusuje makundi makubwa ya ng'ombe kupita ilihali wanajua yanafanya uharibifu?" Anahoji.

Anawauliza inakuwaje makundi ya ng'ombe yatoke Tabora, Kiteto mpaka Morogoro bila kiongozi kufahamu yamefikaje? Tatizo hili linalelewa na 'noti', rushwa, anasema Chongolo na kuelekeza kukamatwa na hatua kali za kisheria zichukuliwe kukomesha hali hiyo.

"Hatua hazichukuliwi ndiyo sababu makundi ya ng'ombe yanaendelea kuranda kwenye makazi kutafuta malisho, kuharibu vyanzo vya maji na mazingira. Viongozi na watendaji wa vijiji wanapewa rushwa kuangamiza kijiji, kuhujumu uchumi bila kujali matatizo wanayopata wananchi," anasema Chongolo.

Anasema pia viongozi wa vijiji wanaachiwa zawadi ya ng'ombe mmoja au wawili mifugo inavyopita katika maeneo yao ili kuwafunga midomo bila kujali athari kubwa wanazolisababishia taifa na kuongeza kuwa viongozi wa vijiji na watendaji, wana tamaa za mali na hiyo sababu ya kuumiza wananchi.

"Mwenyekiti wa kijiji ana ng'ombe wengi, unajiuliza amewatoa wapi, kumbe wanatoka kwa wanaopitisha mifugo, kukiangamiza kijiji, siyo sawa lazima tuseme ukweli na kukemea hili," anasema Katibu Mkuu.

Anaeleza zaidi kuwa, mishahara ya watendaji wa vijiji haiendani na mali wanazomiliki hali inayodhihirisha namna 'wanavyojiongeza' kwenye maslahi binafsi na kuwataka viongozi kueleza ukweli kuhusu sababu zinazochangia mifugo kuhama na migogoro ya ardhi badala ya kufumba macho.

Chongola, anawataka viongozi kuwaelimisha wafugaji kuwa mifugo mingi siyo ufahari, wabadilike na kwamba athari za kumiliki wanyama wengi ni kubwa akiwataka waiuze na kujenga nyumba za kisasa na kusomesha watoto.



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akiwa katika moja ya mikutano mkoani Morogoro. **PICHA: MARY GEOFREY**

### KUKWAMISHA MIRADI

Chongolo anawaonya viongozi na watendaji wa serikali kuwa wanafanya kazi kwa mazoea na kusababisha miradi ya maendeleo kukwama na wananchi kukosa huduma, fedha za serikali kupotea na kuichonganisha serikali na wananchi na kuwapa onyo wanachezea moto.

"Tunataka watendaji wanaosimamia ubora wa kazi na miradi ya maendeleo, thamani ya fedha ionekane. Msicheze na fedha za umma kwa sababu mnacheza na moto," anasisitiza Chongolo.

### MAELEKEZO MADARAJA

Chongolo anatembelea daraja lililoharibiwa na mvua la Nguyami, anaahidi kuhimiza bajeti za ujenzi wa daraja hilo kutengwa pamoja na ujenzi wa madaraja mengine mawili ya Chakwale na Matale.

Anasema madaraja hayo yanayounganisha vijiji na kufungua barabara ya kutoka Gairo kuelekea Kilindi mkoani Tanga, yanapaswa kujengwa haraka iwezekanavyo na kwamba amezungumza na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, anayemhakikishia kuwa wanasubiri bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

Akiwasilisha kilio cha wananchi wa vijiji vinavyonufaika na madaraja hayo yaliyoanguka na mvua, mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby, anasema kutokuwapo kwa miundombunu hiyo, kunababisha adha ya usafiri na kukatika kwa mawasiliamo.

Anasema serikali imeshatoa Shilingi milioni 100 kwa ajili ya usanifu wa ujenzi wa madaraja hayo na kinachosubiriwa ni bajeti kwa ajili ya utekelezaji.

### UMEME NI SHIDA

Jambo lingine analokutana nalo Katibu MKuu ni mkandarasi anayesambaza umeme katika vijiji vya wilaya sita za mkoani Mogorogo kushindwa kufanya kazi kwa weledi. Kampuni ya HNXJDL JV ya China, ndiyo inayodaiwa kushindwa kutimiza wajibu ikidaiwa kusuasua kukamilisha miradi hiyo kwa wananchi na kumtaka ajipange upya vinginevyo sheria itumike kukatisha mkataba wake.

Wananchi wanamweleza kuwa changamoto kubwa ni makandarasi wanaosambaza umeme vijijini kusuasua kutekeleza kazi hizo kwa wakati na wengine kufanyakazi kiholela mfano kuacha nguzo bila kusambaza nyaya kwa muda mrefu.

Akizungumia hilo, Chongolo anasema kero hiyo iko maeneo mbalimbali nchini na haiwezi kuvumilika tena, hivyo kutaka mamlaka Wizara ya Nishati kuvunja mikataba ya makandarasi kama hao na kuwapa kazi wengine wanaowajibika.

INAENDELEA UK. 12

# Vita Russia, Ukraine ni huzuni kwa wajasiriamali kila kona

• Wapo wanaolia kuuza kihasara, wengine waacha biashara

**Na Mwandishi Wetu**

MAPIGANO kati ya Russia na Ukraine yanayotimiza mwaka sasa yakianza Febrauri 2022, yanaendelea kuleta athari za kiuchumi katika mataifa mbalimbali ikiwamo Tanzania ambazo zinawagusa wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo hasa wanawake ambao wameumizwa na mfumuko wa bei.

Wajasiriamali wanaouza magenge na maduka ya vyakula wameathirika zaidi baada ya bidhaa kupanda bei na gharama za usafirishaji kuwa maradufu, anasema Jane Daniel Luakere, anayeuza genge lililoko Nyegezi jijini Mwanza.

Jane anasema mfumuko wa bei umeongeza gharama za usafirishaji na hiyo ndiyo changamoto katika biashara yake hasa kusafirisha bidhaa kutoka soko kuu mpaka anapofanyia biashara na kulazimika kuongeza bei kwa kila kitu anachouza.

"Nalipa fedha nyingi kwenye kusafirisha mzigo tofauti na hapo awali kusafirisha mzigo wa kilo 50 kutoka soko kuu la Nyegezi hadi ninapofanyia biashara umbali wa kilometa mbili natozwa takribani Shilingi 4,000 wakati kipindi cha nyuma ilikuwa 1,000, yote yameongeza gharama za maisha," Jane anaeleza.

Namsifu Gasper, mkazi wa Buguruni Dar es Salaam, ambaye pia ni mfanyabiashara katika soko la Ilala Boma, anaeleza kuwa bidhaa kutoka kwa wakulima zipo juu ukilinganisha na hapo mwanzo, sababu kubwa ni kupanda na bei za pembejeo, vipuri, mafuta na usafirishaji.

"Nauza nyanya katika soko hili la Ilala, kwa zaidi ya miaka mitano, jambo linalonishangaza sasa ni gharama za vitu kupanda sokoni, boksi la nyanya siku za nyuma linauzwa Shilingi 30,000 leo ni 70,000 jambo linalonilazimu kuuza sado moja kwa Shilingi 5,000 hadi 6,000 badala ya 2,000 za miaka miwili iliyopita." Namsifu anasema.

Anaongeza kuwa ongezeko la gharama za usafirishaji, pembejeo na bidhaa za kilimo umemwondoa kwenye uuzaji wa viazi mbatata, japo amefanya biashara hiyo kwa muda mrefu lakini gharama za manunuzi zimemlazimisha kuacha biashara hiyo.



Wafanyabiashara na wateja sokoni wana kilio cha ongezeko la bei za bidhaa kutokana na mfumuko wa bei. **PICHA: MTANDAO**

> Aidha, inazikumbusha nchi hizo kuwa wakati umefika wakujitazama kwa kila kitu kuanzia chakula, nishati, huduma na teknolojia ili kupunguza utegemezi.

"Gunia moja la viazi linafika 120,000 kwa sasa, wakati hapo mwanzo tulikuwa tunanunua 70,000 hivyo ili kupata faida itanilazimu kuuza sado 7,000 ila ninauza kwa 5,000 na kuanguka kibiashara tukiwauliza wakulima wanasema gharama za usafirishaji ziko juu kutokana na bei ya petroli , vipuri na vilainisha kuongezeka mno," anasema Namsifu.

Angelus Mgobe ni dereva wa bodaboda, anayejishughulisha na kubeba mizigo katika soko la Buza Dar es Salaam, anakiri kupandisha gharama za kusafirisha kwa sababu ya ongezeko la bei ya mafuta ikilinganishwa na hapo mwanzo.

"Bei ya petroli ilianza kupanda kama utani, kisha ikashuka lakini bado iko juu hali inayoendelea kutuathiri wajasiriamali, mara kadhaa najikuta nikipata hasara pale ninapokuwa namsafirishia mteja kwa bei ninayoona itanilipa, naye mteja kukataa kutoa fedha hiyo kwa kuona kama analanguliwa, haya yote yanasababishwa na vita vya vilivyosababisha bei ya mafuta kuwa juu," anaongeza.

Mchambuzi wa masuala ya uchumi Ally Mkimo, akizungumza na Nipashe anasema Urusi ni kati ya nchi zinazosifika kwa uzalishaji na usambazaji wa mafuta kwa wingi duniani ikichangia kwa zaidi ya asilimia 30 na kwamba vita vinavyoendelea vinazidisha kupanda kwa gharama za bidhaa kutokana na kuongezeka gharama za uendeshaji zinazosababishwa na mafuta kupaa.

"Kina mama lishe na wajasiriamali wengine wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na vita hivi kwa kuwa wanategemea mazao ya chakula kutoka kwa wakulima ili waweze kufanya biashara zao jambo ambalo linaongeza gharama zinapotoka shambani zinakuwa juu hata zinapopokelewa sokoni kwani mbolea na viuatilifu vingi vinavyotoka nje.

Mkimo anaeleza kuwa kutokana na bei ya mafuta kupanda inasababisha mnyonyoro wa gharama kuanzia kwa mkulima na usafirishaji hadi bidhaa hiyo inapofika sokoni, kuongezeka na hiyo inamaanisha kuwa mtu wa mwisho lazima alipe zaidi na kujikuta akitumia hela nyingi kununua bidhaa hiyo hali inayosababisha kinamama wengi kujikuta wakifunga biashara zao na wengine mitaji yao kuyumba kutokana na gharama za usafirishaji.

**ATHARI CHANYA**

Mchambuzi huyo wa uchumi, pia anaeleza athari chanya zilizoonekana baada ya vita hivyo kuwa ni mwamko kwa nchi za Afrika kufahamu kwamba, zinatakiwa kuwekeza zaidi kwenye sekta ya kilimo na vilevile kwenye nishati hasa gesi ili kujitosheleza wenyewe pasipo kuwa na utegemezi mkubwa wa bidhaa kutoka nje.

Aidha, inazikumbusha nchi hizo kuwa wakati umefika wakujitazama kwa kila kitu kuanzia chakula, nishati, huduma na teknolojia ili kupunguza utegemezi.

Meneja Masoko Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam, Anthamin Mandari, anakiri bei za bidhaa kuwa juu katika soko la Temeke nakueleza kuwa sababu ya ukame katika baadhi ya mikoa wazalishaji inaweza kuwa chanzo kikubwa pia.

Halikadhalika, Mandari anaeleza kuwa mabadiliko ya dunia yaliotokea kama vita vya Urusi na Ukraine yameongeza mfumuko wa bei za mafuta na kusababisha shida ya gharama ya mafuta kupanda na gharama zingine kuendelea kuwa juu.

Urusi na Ukraine ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa uzalishaji wa mafuta na nafaka. Baadhi ya mataifa mbalimbali ikiwamo Afrika zimekua zikitegemea bidhaa kutoka katika nchi hizo hivyo kukumbwa na athari nyingi zinazotokana na za vita hivyo.

## Viongozi, watendaji waangamiza vijiji kisa? Hongo za mifugo, fedha

**INATOKA UK. 11**

Aidha, Chongolo anamwagiza Wakala wa Umeme Vijijini (REA), kupeleka mkandarasi kwa ajili ya kusambaza umeme kwa wananchi katika Kijiji cha Itaragwe. Anaeleza kuwa katika vijiji 179 vinavyopaswa kufunga umeme ni viwili pekee ambavyo vimepata huduma hiyo na kuagiza hadi Februari 15, mwaka huu, mkandarasi awe ameanza kufanya kazi vinginevyo atanyang'anywa zabuni hiyo na kupewa mwingine atakayeendana na kasi inayotakiwa.

Kwenye maji Chongolo anaagiza TANESCO, kufunga umeme badala ya jenereta zinazotumiwa sasa kusukuma maji kutoka kwenye chanjo hicho ili kuwapunguzia wananchi gharama kubwa za kununua maji.

Meneja TANESCO mkoani humo, Fadhili Chilombe, anamhakikishia Chongolo kuwa watakamilisha kazi hiyo ndani ya mwezi mmoja.

**WALIMU VIJIJINI**

Aidha, Chongolo anaiagiza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupanga walimu kufundisha shule za vijijini ambako kuna uhitaji badala ya kurundikana maeneo ya mijini.

Anasema serikali imejenga madarasa ya kutosha kwa ajili ya wanafunzi kusoma lakini shule za vijijini hazina walimu wa kutosha jambo ambalo halikubaliki na kuwataka

pia viongozi na watendaji wa mkoa huo, kujitathmini kuhusu kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mkoa huo.

**UTATUZI KERO**

Katibu wa Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema, anawaahidi wanachama wa CCM wilayani Gairo, Mvomero na Kilosa kuwa, ziara hiyo itahakikisha inafanikisha utatuzi wa kero za wananchi kwa asilimia 70.

Anawataka wajumbe wa mashina, kufanya vikao vya mara kwa mara kwa ajili ya kujadili maendeleo, kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za wananchi katika maeneo yao na kuwataka watendaji waliopewa dhamana ya kuongoza wananchi katika maeneo mbalimbali, kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

# Je, SMZ inazikumbuka ahadi ya kurekebisha sheria kandamizi?

## • Wanahabari watoa neno kwa Rais Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kulinda wanahabari na uhuru wa vyombo vya habari ili kufanya kazi kwa ufanisi, wadau wa tasnia ya habari wanasisitiza kuwa ni vyema sheria kandamizi zinazoubinya uhuru huo kurekebishwa.

Miongoni mwa sheria ambazo zinaminya uhuru wa habari Zanzibar ni Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya Mwaka 2017 ni kwa mujibu mwandishi mbobezi, Salim Said Salim.

Akizungumza katika mkutano wa kujadili sheria zinazokandamiza tasnia ya uhuru wa habari, Salim anasema zipo nyingi ambazo zinahitaji kupitiwa na kufanyiwa marekebisho, hatua ambayo itawawezesha wanahabari kutekeleza majukumu yao bila ya vikwazo na kuifikishia jamii habari kikamilifu.

Anasema miongoni mwa sheria ambazo zinahitaji marekebisho ni Sheria ya Uchaguzi ya Uchaguzi ya Zanzibar mwaka 2017, ambayo ina vifungu kadhaa vinavyokandamiza uhuru wa habari. Kwa mfano, anasema kifungu cha 127 (1) kinachohusu utangazaji wa matokeo kinyume na sheria, kinafaa kufutwa kwa sababu kinawanyima wananchi haki ya kupata matokeo ya uchaguzi hata yale yaliyobandikwa katika kuta kwenye vituo vya kupigia kura.

"Kama matokeo hayo yamebandikwa katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya wananchi kufahamu ni vipi liwe kosa, zile ni nyaraka za umma ambazo wananchi wana haki ya kupewa taarifa zake kupitia waandishi wa habari, lakini sheria inanyima fursa hiyo hadi msimamizi wa uchaguzi atangaze," anasema.

Kifungu hicho cha sheria kinawabana wanahabari uhuru wa kutoa taarifa kwa umma kwa hivyo kinahitaji kurekebishwa, ambayo yatakwenda sambamba na utekelezaji wa ufanisi wa majukumu yao, akiongeza kuwa kipengele hicho mwandishi atakayetoa taarifa za matokeo kwa kufanya majumuisho atakuwa ni mtuhumiwa, akipatikana na hatia anaweza kutumikia kifungo kisichopungua miezi 30 (miaka 2.5).

"Kwa kuwa maofisa wa Tume ya Uchaguzi ndiyo waliojumulisha taarifa hizo kwa kuzihakiki na baadaye kuzibandika ubaoni au ukutani katika vituo kuna ubaya gani kwa waandishi kuzitoa hizo kwa umma?" Anahoji.

Anasema utaratibu huo ni tofauti na nchi jirani kama Kenya, ambako vyombo vya habari vinashirikishwa kwa karibu katika kupiga kura na kutangaza matokeo, akitolea mfano wa uchaguzi mkuu wa Agosti mwaka jana 2022.

Shifaa Said, mwandishi wa habari mwandamizi anasema tangu mwaka 2010 wanapigania mabadiliko ya sheria zinazokinzana na uhuru wa habari lakini bado hazijarekebishwa.

"Sisi wadau wa habari hatuchoki kupiga debe ili sheria hizi ikiwamo ya uchaguzi kufanyiwa marekebisho ili waandishi wafanye kazi zao kwa ufanisi na jamii ipate taarifa sahihi kwa wakati mwafaka," anasema.



Wanahabari wakiwa kwenye mjadala wa sheria kandamizi kwa tasnia ya habari katika Ofisi za TAMWA, Tunguu Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

> Kwa kuwa maofisa wa Tume ya Uchaguzi ndiyo waliojumulisha taarifa hizo kwa kuzihakiki na baadaye kuzibandika ubaoni au ukutani katika vituo kuna ubaya gani kwa waandishi kuzitoa hizo kwa umma?

Anasema kupitia mradi unaotekelezwa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA-Zanzibar) na Shirika la Internews wamezipitia na kuzifanyia uchambuzi wa kina sheria nane ambazo zinakandamiza uhuru wa habari Zanzibar ikiwamo ya Uchaguzi ya Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu ya mwaka 1988 na Sheria ya Utangazaji ya mwaka 1967.

Anasema kipengele cha 123 cha Sheria ya Uchaguzi kinakataza mtu yeyote kutoa taarifa za matokeo ya uchaguzi yaliobandikwa katika vituo vya kupigia kura bila ya idhini ya Tume ya Uchaguzi na kinakizana na kanuni ya uwazi na uwajibikaji kwa sababu kuwekwa matokeo ukutani, inamaanisha kwamba nyaraka tayari zimetambulishwa kuwa ni za umma hivyo kuwazuia waandishi wa habari kuchapisha matokeo ni kukandamiza vyombo vya habari na uhuru wa habari.

Anasema sheria hiyo inaeleza kuwa endapo mwandishi atafanya kinyume na sheria hiyo ni kosa na adhabu yake atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Juma Khamis, mkufunzi wa wanahabari katika masuala ya sheria, anasema pia kifungu cha 127 cha sheria hiyo ya uchaguzi kunaminya uhuru wa habari ambapo kimeeleza ni marufuku kwa mgombea, chama cha siasa, taasisi au mtu mwingine yeyote, kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi.

Anasema ni vyema kifungu hicho kikaainisha moja kwa moja taasisi au kundi la watu badala ya kusema yeyote kwa sababu kubaki hivyo kifungu hicho kinawahusisha mpaka wanahabari.

"Ni vyema kipengele hiki kikafanyiwa marekebisho ili kieleze wazi ni watu wa aina gani wasiopaswa kufanya hivyo kuliko kusema ni yeyote ambapo waandishi wa habari pia wanajumuishwa,"anasema.

Aidha, kifungu hicho pia kinaeleza kuwa mgombea, chama cha siasa, taasisi au mtu mwingine atakayetangaza matokeo ya uchaguzi au kuitaka tume kutangaza matokeo kabla ya kuishi kwa muda wa kutangaza matokeo uliopangwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani adhabu yake ni faini ya Shilingi milioni 100 au kifungo cha miezi 30 jela.

Mkufunzi huyo ambaye ni mtaalamu wa sheria, anashauri haja ya kufanyika marekebisho ili kutoa fursa kwa wanahabari kutekeleza wajibu wao kwa kupata uhuru zaidi.

Baadhi ya wadau wa habari wanasema baadhi ya nchi za Afrika mfano Nigeria, Kenya na mashirika nchini Afrika Kusini yanafanya hesabu zao yenyewe kutangaza matokeo bila kizuizi chochote.

Dk. Mzuri Issa Mkurugenzi wa TAMWA-Zanzibar, anasema hata hivyo, wadau wana nafasi kubwa ya kuendelea kutetea uhuru wa habari kwa kushirikiana na wawakilishi, asasi za kiraia na mashirika ya kimataifa.

Anasema uhuru wa habari ni nguzo muhimu katika maendeleo ya taifa na unafanikisha kukuza uchumi na maendeleo kwenye nchi hivyo inapotokea sheria ya tasnia hiyo kubana uhuru huo ni vyema kufanyiwa marekebisho.

Anasema kuna kila sababu ya kuona kwamba sheria, sera na matendo yaendane na mikataba ya kimataifa kuhusu uhuru wa habari ili kuleta maslahi kwa makundi yote.

Anasema azimio kubwa la haki za binadamu la umoja wa mataifa ambalo lilitoka mwaka 1948 ambalo limeweka misingi mikubwa ikiwamo kila mmoja anahaki ya kutoa maoni na kujieleza bila ya kuingiliwa na kupokea taarifa na kueneza kupitia vyombo vya habari bila ya vikwazo.

Anasema Tanzania inapaswa kutekeleza hayo kwa sababu imeridhia mikataba hiyo ya kimataifa na kuna kila sababu ya sheria, sera na matendo kuendana na mikataba hiyo.

Aidha anawataka wanahabari kuendelea kufanya ushawishi wa mabadiliko ya sheria kwa kuandika upungufu uliyoko katika sheria hizo ili kufanyiwa marekebisho kwa haraka.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati anawaapisha mawaziri aliowateua, alisema kama kuna sheria kandamizi ni vyema viongozi kushirikiana na wadau kuzifanyia marekebisho ili kuongeza ufanisi.

"Kama mnahisi kuna sheria ambazo zimepitwa na wakati au zinakinzana katika ufanisi wa kazi zifanyieni marekebisho ili ziendani na wakati tulionao,"anasema Dk. Mwinyi.

MARTIN LUTHER KING JR
'NINAYO NDOTO'

# Maono yake yanavyobaki kuwa fikra inayoishi kwa wanasiasa, wanaharakati



Ni mafuriko kutokana na umati uliomiminika kwenye mikutano ya Martin Luther King Jr, alipokuwa jukwaani. **PICHA: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

MARTIN Luther King Jr, anakumbukwa na kuheshimika kuwa mpiganiaji wa haki za kiraia akijikita kupambana na umaskini na ukosefu wa usawa miongoni mwa Waamerika weusi.

Anabakia kuwa nyenzo muhimu leo kama ilivyokuwa wakati wa harakati za haki za kiraia kwa za Waamerika.

Yapo mengi aliyofanya ambayo dunia inaendelea kumkumbuka na kuyaenzi na kila zikisikika hotuba alizohutubia alitumia kauli ya 'nina ndoto' akitarajia mengi, kutokana na wakati huo nchi ya Marekani kukithiri kwenye ubaguzi wa rangi na unyanyasaji wa watu weusi wanaoitwa hata leo 'nigers'.

Mwaka 1963, mwimbaji wa nyimbo za Injili Mahalia Jackson, alipaza sauti akisema "Waambie kuhusu ndoto hiyo, Martin!"

Mwito huo ulimsukuma, Martin Luther King kuelekeza kwenye mahubiri ya awali aliyotoa na akiandika kwenye toleo la American Dream ambalo lilikuwa ni usawa na kufikiwa na wananchi wote.

"Nina ndoto kwamba watoto wangu wadogo wanne siku moja wataishi katika taifa ambalo hawatabaguliwa kwa rangi ya ngozi zao, bali kwa tabia zao. Nina ndoto leo," alieleza.

Januari mwaka 2009, inaweza kuwa ndio ndoto aliyoiota Martin Luther King Jr kutimia, baada ya Barack Obama kuwa Rais wa 44 wa Marekani.

Ni Mwafrika-Mwamerika wa kwanza kushika wadhifa huo, na pia mtu wa kwanza mwenye kuzaliwa Hawaii, kuwa kiongozi wa taifa hilo ambalo weusi kwa muda mrefu hawana haki kama ilivyo kwa weupe.

> "Nina ndoto kwamba watoto wangu wadogo wanne siku moja wataishi katika taifa ambalo hawatabaguliwa kwa rangi ya ngozi zao, bali kwa tabia zao. Nina ndoto leo.



Ndoto yake ya usawa ni ya Marekani. "Licha ya kudharauliwa kwake, Martin Luther King alifanya kazi kubwa ya kujaribu mara kwa mara nyingi kuonyesha jinsi juhudi zake zilivyolingana na maadili ya Marekani," anasema Lerone Martin, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti na Elimu ya Martin Luther King Jr katika Chuo Kikuu cha Stanford.

Baada ya kuzaliwa Januari 15, mwaka 1929, alipewa jina la babake, Michael King. Lakini miaka sita baadaye, baba yake (Martin) alitembelea Ujerumani na kupata habari kuhusu mtu aitwaye Martin Luther, kiongozi wa mageuzi ya Kiprotestanti ya kutaka mabadiliko kwenye mafundisho ya Injili.

Na mara aliporejea nyumbani inasemekana kuwa alitiwa moyo sana na alibadilisha rasmi majina ya mtoto wake mkubwa kuwa Martin Luther King.

Mwaka 1944, Martin Luther King Jr alidahiliwa katika Chuo cha Morehouse akiwa na umri wa miaka 15. Vizazi vya familia ya King walikuwa wamehitimu kutoka chuo kikuu cha kihistoria cha wanaume weusi huko Atlanta, Georgia.

Kulingana na Taasisi ya King, kiongozi wa baadaye wa haki za kiraia alisemekana kuwa mwanafunzi wa "kawaida", lakini wakati wake huko Morehouse ulikuwa muhimu katika kuamsha shauku yake ya usawa wa kijamii na kisiasa na kumtia moyo kuwa mhubiri.

### AKAMATWA MARA KADHAA

Katika miaka yake 13 kama kiongozi wa haki za kiraia, Martin Luther King Jr alikamatwa mara 30, hasa kwa makosa na ukiukaji wa maandamano ya raia, kwa mujibu wa maelezo ya Kituo cha King.

Ingawa mara nyingi alikuwa mlengwa wa vyombo vya usalama, hakufurahia kufungwa, Oktoba mwaka 1960 baada ya maandamano ya kuketi katika duka kubwa huko Atlanta alishikiliwa katika gereza la jimbo la Georgia.

Alimwandikia mke wake, Coretta, kutoka jela akisema kwamba anatumaini mateso ambayo sasa yanakuja kwa familia yetu yatasaidia kwa njia fulani kufanya Atlanta kuwa jiji bora, Georgia jimbo bora na Amerika kuwa nchi bora."

### MWANDISHI VITABU

Kituo cha Martin Luther King, kinasema kuwa aliandika vitabu vitano katika kipindi cha maisha yake na kuchapisha makusanyo mengi ya barua na mahubiri yake.

Kitabu chake cha mwaka 1964, kiliitwa 'Why We Can't Wait', kilisimulia matukio yaliyosababisha kampeni ya kihistoria ya Birmingham, Alabama, kukomesha ubaguzi. Watoto wa Martin Luther King, Malcolm X na Kwame Nkrumah walielezea hali ya ubaguzi Marekani.

Septemba mwaka 1958, Martin Luther King alikaribiwa na mwanamke mwenye matatizo ya akili, alipokuwa akitia saini nakala za kitabu chake kipya zaidi 'Stride Toward Freedom' huko Harlem.

Mwanamke huyo alithibitisha kwamba kweli alikuwa mfalme kabla ya kumchoma kwa kifaa chenye urefu wa inchi saba. Wakati huo, madaktari walisema aliponea chupuchupu kufa, kwa sababu kisu kilikuwa karibu sana na mshipa mkuu wa damu 'aorta' taarifa zinazotolewa na Taasisi ya Martin Luther King.

Baada ya kujua kwamba mwanamke huyo alikuwa mgonjwa wa akili, alisema: "Sina uchungu juu yake" na badala yake akatoa wito apokee matibabu ya akili.

### MAMA KUUAWA

Juni 30, mwaka 1974, miaka sita baada ya kuuawa kwa Martin Luther King Jr, mwanamume mwenye umri wa miaka 23 alimpiga risasi na kumuua mama yake.

Alberta Williams King, alipokuwa akipiga ala ya muziki wakati wa ibada katika Kanisa la Ebenezer Baptist, alifarikia dunia.

Mshambuliaji huyo alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifo, lakini baadaye alihukumiwa tena kifungo cha maisha jela kwa sababu ya upinzani wa familia ya Martin Luther King dhidi ya hukumu ya kifo.

Martin Luther King Jr, alikuwa na umri wa miaka 39 alipouawa, ikiwa ni Aprili 4, 1968. Alitumia miaka 13 mbele ya umma akipigania haki za kiraia na usawa wa rangi.

Lakini kwa mujibu wa Kituo cha King katika muda huo mfupi alileta maendeleo zaidi kuelekea usawa wa rangi nchini Marekani kuliko miaka 350 iliyopita.

**CHANZO BBC**



# Kiwango cha maadili watumishi wa umma chazidi kuongezeka

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

KIWANGO cha uzingatiaji wa maadili kwa watumishi wa umma kimeongezeka kwa asilimia 9.8 ndani ya miaka nane, huku maeneo matano yakitajwa kuongoza kwa kulalamikiwa zaidi kukithiri kwa uvunjifu wa maadili.

Katika utafiti wa hali ya uadilifu na uzingatiaji wa maadili kwenye utumishi wa umma mwaka 2022, kiwango hicho kimeongezeka kutoka asilimia 66.1 mwaka 2014 hadi asilimia 75.9 mwaka 2022.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ameagiza wadau wa usimamizi wa maadili katika utumishi wa umma kujadili kwa kina na kutoa mapendekezo kuhusu sababu za taasisi hizo kuendelea kuwa na viashiria vya uvunjifu wa maadili.


Akifungua kikao cha wadau hao jana, Mhagama alisema maeneo hayo matano yanayolalamikiwa zaidi kwa kukithiri kwa viashiria vya uvunjifu wa maadili kuwa ni polisi, mahakama, manunuzi ya umma, huduma za ardhi na mikataba mbalimbali.

"Katika utafiti huu uliofanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) maeneo haya kama polisi, mahakama na huduma za ardhi zinajirudia, nitoe wito kwenu kwenye kikao hiki mwangalie matokeo haya kwa kina na mbainishe ni nini sababu ya taasisi hizi kuendelea kuwa na viashiria vya uvunjifu wa maadili,"alisema.

Alisema bado kuna maeneo yanahitaji kuboreshwa au kutiliwa mkazo ikiwamo ufuatiliaji wa kila mara wa uzingatiaji wa kanuni za maadili kwa watumishi wa umma.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Xavier Daud, alisema kikao hicho ni utekelezaji wa maagizo ya Waziri Mhagama aliyetaka kiitishwe ili kufanya majadiliano ya kina kuhusu matokeo ya utafiti huo na kuja na mikakati ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili katika sekta zote kulingana na matokeo.

Awali, Mkurugenzi wa Usimamizi Maadili wa Ofisi hiyo, Leila Mavika, alisema utafiti huo ulilenga kuangalia wananchi wanaridhika na huduma wanazopata na kama watumishi wanaotoa huduma wanatimiza wajibu wao, ili serikali ichukue hatua stahiki.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akimwapisha Mbunge Mteule wa Jimbo la Amani, Abdul Yussuf Maalim, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waganga wakuu mikoa, wilaya watakiwa kujitafakari

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amewataka waganga wakuu wa mikoa na wilaya kujitafakari kutokana na kuwapo vitendo vya ubadhirifu katika vituo vyao vya kazi.

Dk. Mollel alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akisoma tamko kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika kilele cha Siku ya Ukoma Duniani ambayo hufanyika kila Jumapili ya mwisho ya Januari.

Dk. Mollel alisema kuwa pamoja na serikali kuwekeza zaidi katika sekta ya afya kwa kuongeza majengo vifaa vya kisasa lakini bado kuna tatizo kubwa kwa uboreshaji wa huduma ya afya kwa watendaji.

"Inasikitisha kumkuta Mganga Mkuu wa Mkoa, Wilaya au wa kituo wanapokwenda viongozi wa juu kutoka serikalini au wizara na kukuta madudu, wakiwa wanashangaa na hata naye Mganga Mkuu wa Mkoa na Wilaya na wao wanashangaa."

"Jambo hilo haliwezi kuvumiliwa na kama itaendelea kuwa hivyo nitalazimika kuwabutua kwani kila mmoja anatakiwa kucheza mpira kwa namba yake na si vinginevyo," alisisitiza Dk.Mollel.

Aidha, aliwaomba waganga wakuu wa mikoa na wilaya wanapopokea dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ni vyema wakashirikisha wakuu wa wilaya na mikoa kwa kuwa hao ni wenyeviti wa kamati ya ulinzi na usalama kwa lengo la kuboresha usimamizi katika sekta ya afya.

Alisema ili kuboresha usimamizi wa huduma za afya pande zote hizo zinatakiwa kushirikiana kwa pamoja ili ubora wa huduma za afya uendelee kustawi.

Kuhusu kilele cha Siku ya Ukoma Duniani, Dk. Mollel alisema kuwa kwa sasa Tanzania imepiga hatua katika kupambana na ugonjwa huo.

Alisema kuwa ugonjwa wa ukoma nchini umepungua mwaka hadi mwaka katika miongo miwili iliyopita ambapo dunia iliongeza kasi ya kupambana nao.

Alisema kuwa Tanzania tayari imefikia hatua ya awali ya kiwango cha kimataifa cha utokomezaji wa ukoma na kuwa chini ya mgonjwa mmoja kati ya watu 10,000.

"Hatua zinazofuata ni kutokuwa na mtoto anayeugua ukoma nchini kwa miaka mitatu, mitano na hatimaye 10 mfululizo kwa mwaka 2021 watoto waliogundulika kuugua ukoma ilifika 41 na hivyo kuonesha wazi ya kuwa mnyororo wa maambukizi bado upo na bado tuna jukumu kubwa la kufanya kukomesha kuenea kwa ugonjwa huo na kwa sasa wagonjwa wengi wanaogundulika ni wale wa zamani," alisema Dk. Mollel.

Dk. Mollel alitaja mikoa mbayo imekuwa na wagonjwa wengi wa ukoma kuwa ni Morogoro, Lindi, Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Tanga, Katavi, Dodoma, Geita, Shinyanga, Tabora na Rukwa.

Aliagiza kila halmashauri kujumuisha shughuli za kutokemeza ugonjwa wa ukoma katika mikakati mingine ya afya.

Vilevile alisema mikoa na halmashauri kuhakikisha kila mgonjwa anayeibuliwa anatambuliwa anakotoka.

## Serikali yawahakikishia usalama mabalozi, wakuu mashirika

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

SERIKALI imewahakikishia mabalozi na wakuu wa mashirika ya kimataifa duniani kuwa Tanzania ni salama.

Imesema kuwa jukumu la kutoa taarifa ya hali ya usalama wa nchi ni la serikali siyo vinginevyo na kama mtu ataona kuna viashiria vya aina yoyote anapaswa kutoa taarifa kwa mamlaka husika badala ya kusambaza uvumi ambao unaleta taharuki.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, alibainisha hayo juzi jijini hapo, alipokuwa akizungumza na mabalozi wa nchi mbalimbali na wakuu wa mashirika ya kimataifa kuhusu hali ya usalama nchini.

"Wiki iliyopita kulikuwapo na uvumi kuwa kuna matishio ya vurugu ndani ya nchi yetu hadi Shirika la Ndege la KLM, kusitisha safari zake nchini, serikali ilianza kuzifanyia kazi na polisi walitoa taarifa, hata Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alitoa taarifa kuwa anga letu ni salama.

"Kutokana na hali hiyo leo hii tumewaita wadau wa maendeleo wakiwamo mabalozi na kuwahakikishia kuwa hali yetu ni salama kabisa hakuna tishio lolote la kiusalama tunawahakikishia Watanzania na dunia kwa ujumla kuwa Tanzania ni salama na tuwashukuru wale wote hata uwepo wa taarifa hizo waliendelea kuja nchini," alisema.

Pia alisema katika kikao hicho na wadau hao wamekubaliana kuwa hali hiyo haitajitokeza tena na wataendelea kufanya kazi kwa kushirikiana.

Alisema baadhi ya mabalozi wamemweleza kuwa tayari wameshatoa taarifa katika nchi zao kuwa Tanzania ni salama na hakuna tishio lolote la kiusalama.

"Siwezi kusema kuwa aliyetoa taarifa hizi alikuwa na nia gani lakini kikubwa ni kwamba tumekubaliana kuwa hali kama hii haitajitokeza tena na sitarajii hali hii kujirudia tena kutokana na makubaliano ya kikao hiki ambacho kimehusisha mabalozi wenyewe na wakuu wa mashirika ya kimataifa karibu nchi zote,"alisisitiza.

Alisema suala la ulinzi na usalama ni lazima kushirikiana hivyo wamekubaliana katika mambo ambayo wanapaswa kufanya kwa pamoja ni lazima kuyafanya katika njia zinazofaa na siyo njia ambazo zitaleta taharuki kwa Watanzania na nchi nyingine.





# Mkandarasi hatarini kuporwa zabuni kisa ucheleweshaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKANDARASI anayesambaza umeme vijijini katika Mkoa wa Mbeya, yuko hatarini kuporwa tenda hiyo baada ya serikali kueleza kutoridhishwa na kasi ya utendaji kazi wake huku ikimpa miezi miwili ya kujitathmini.

Mkandarasi huyo ni Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme (ETDCO) ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme nchini (TANESCO).

Kampuni hiyo iliingia makubaliano na Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) kusambaza umeme kwenye vijiji 139 vya Mkoa wa Mbeya miaka miwili iliyopita lakini mpaka sasa imewasha umeme kwenye vijiji 19 pekee huku muda wa mkataba ukiwa umekwisha.

Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa REA, Mhandisi Jones Olotu, alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha tathmini ya usambazaji wa umeme mkoani Mbeya kilichowashirikisha wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya REA, mkandarasi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Alisema kwa mujibu wa mkataba wa mkandarasi huyo ulikuwa wa miezi 18 na ulitakiwa kukamilika Februari 2, mwaka huu, lakini mpaka sasa amekamilisha kazi kwenye vijiji 19 pekee jambo ambalo limesababishwa na uzembe.

Alisema kutokana na hali hiyo mkandarasi huyo amepewa nyongeza ya miezi nane na kwamba Waziri wa Nishati, Januari Makamba, amempa miezi miwili mkandarasi huyo kujitathmini kama anaweza akaendelea na kazi hiyo ama asitishiwe mkataba.

"Sisi mpaka sasa haturidhishwi na utendaji wa mkandarasi huyu maana kasi yake ni ndogo sana, tumefanya naye vikao vingi lakini hatuoni mabadiliko, lakini Waziri wa Nishati amefanya naye kikao ambacho amempa miezi miwili ya kujitathmini," alisema Mhandisi Olotu.

Meneja wa Mradi huo, Mhandisi Mustapher Himba, alisema awali walipewa vijiji 114 lakini baadaye vikaongezeka na kufikia 139 na hivyo wakaomba kuongezewa muda ili kukamilisha kazi hiyo.

Alisema kwa sasa wana mpango wa kuhakikisha wanawasha umeme kwenye vijiji 95 kufikia Mei mwaka huu ili vijiji 44 vitakavyokuwa vimebakia viwashwe kati ya mwezi Juni na Julai ambao ndio utakuwa mwisho wa mkataba.

Alisema mpaka sasa wameshafunga transfoma kwenye vijiji 35 ambavyo vinasubiri ukaguzi wa mkandarasi mshauri ili viwashwe kabla ya kuendelea na maeneo mengine.

Alisema ili kuendana na kasi ya mradi huo, kampuni imeongeza wasambazaji wa vifaa na upelekaji wa vifaa kwenye vijiji ili kazi ifanyike kwa wakati hasa kwenye vijiji 95 vya awali.

"Matatizo yaliyosababisha mradi uchelewe kukamilika ni kama kupanda kwa bei ya chuma na wazalishaji wa nguzo kushindwa kuzalisha kwa wakati kutokana na kukosekana kwa kemikali lakini kwa sasa tumeshanunua vifaa vipo Dar es salaam vinaendelea kuletwa," alisema Mhandisi Himba.

Florian Haule ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa REA, alimuomba Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera kusaidia kumsimamia mkandarasi huyo ili akamilishe kazi hiyo na wananchi waanze kupata huduma.

Alisema bodi hiyo hairidhishi kuona wananchi wanachelewa kuanza kupata huduma wakati serikali ilishatoa fedha kwa ajili ya kuwasambazia nishati hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera alisema hata yeye haridhishwi na kampuni hiyo na hivyo akaitaka kujitathmini kabla haijachukuliwa hatua za mikataba ikiwamo kuvunjiwa mkataba na kumtafuta mkandarasi mwingine.

Aliiagiza impelekee ratiba ya uwashaji umeme kwenye vijiji vyote ili ratiba hizo zibandikwe kwenye ofisi za kata husika na wakuu wa wilaya wajiandae kwenda kuwasha.

Kwa mujibu wa mkataba wa kampuni hiyo ni kwamba gharama za usambazaji wa umeme kwenye vijiji vyote mkoani Mbeya ni Sh. bilioni 40.8.



Baadhi ya madiwani wakifuatilia mkutano wa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023 wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Watu wanne wakamatwa wakiingiza mayai njia za panya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuingiza nchini mayai ya kuku wa kienyeji kutoka nchi jirani kupitia njia za panya ili kukwepa ushuru wa kuingiza bidhaa hiyo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni mbalimbali zilizofanywa na jeshi hilo katika maeneo tofauti.

Kamanda Kuzaga aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ibrahimu Mwaiteke (41), Taifa Jackson (24), Lucas Paul (23) na Solo Mwakajinga (40) ambao wote ni wakazi wa Wilaya ya Kyela mkoani humo.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiingiza nchini makasha 112 ya mayai hayo kutoka Malawi na kwamba mayai hayo yanakadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 2.5.

"Baada ya kuyaingiza nchini mayai hayo walitaka kuyasafirisha kwa kutumia gari yenye namba za usajili T.714 DLE aina ya Toyota Coaster lakini kutokana na umahili wa askari wetu wa eneo hilo watuhumiwa walikamatwa na kupelekwa kituoni," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema watuhumiwa wanaendelea kushikiliwa kituoni wakati uchunguzi unaendelea ili afikishwe mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuepuka kufanya biashara za magendo kwa maelezo kuwa zitawasababishia umaskini kutokana na mali zao kutaifishwa.

Alisema kwa sasa makachelo wa jeshi hilo wamebaini vipenyo vyote visivyokuwa halali vinavyotumika kuvusha magendo na hivyo wataweka mitego kwenye vipenyo hivyo ili kuwanasa zaidi wasafirishaji hao wa magendo.

# Serikali yamaliza mgogoro kati ya kijiji na Bodi ya Maji

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

SERIKALI mkoani Mbeya imemaliza mgogoro wa ardhi uliokuwa unaendelea kati ya wananchi wa Kijiji cha Ikama Kata ya Itagata wilayani Rungwe na uongozi wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa ulioanza kufukuta mwaka jana.

Mgogoro huo ulianza baada ya bodi hiyo kusimika mawe kwenye mashamba ya wananchi kwa ajili ya kuwazuia wasiendelee na shughuli za kilimo kwa ajili ya kupisha uhifadhi wa chanzo cha maji cha Mto Mbaka ambapo zaidi ya ekari 57 za wananchi zilichukuliwa.

Kufuatia hali hiyo wananchi wa kijiji hicho walipandwa na hasira na wakang'oa alama zote zilizowekwa na bodi hiyo na kisha wakaendelea na shughuli za kilimo kwenye maeneo hayo.

Mwishoni mwa wiki Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilifika katika kijiji hicho kwa ajili ya uzinduzi wa upandaji wa miti na kutatua mgogoro huo ambapo iliamuru bodi hiyo kufanya tathmini ili wananchi hao walipwe fidia.

Homera aliitaka bodi hiyo kuacha kuvamia mashamba ya wananchi bila kuwashirikisha kwa maelezo kuwa hali hiyo inasababisha migogoro isiyokuwa na sababu.

Alisema serikali haikuwa tayari kuona wananchi wakinyanyaswa kwenye maeneo yao kwa kuporwa mashamba yao na badala yake inataka taratibu zifuatwe wakati wa kuyatwaa maeneo hayo ili na wao waridhie kutoka.

Alisema wananchi hao ndio walinzi wa chanzo cha maji hayo na hivyo endapo wangeshirikishwa mapema wasingezing'oa alama zilizowekwa kwenye maeneo yao.

"Kwanza nawapongeza wananchi kwa kuzing'oa alama hizo kwa sababu hawakufuata utaratibu, lakini sasa hivi naomba mzirejeshe ili maeneo yenu yafanyiwe tathmini na mlipwe fidia, serikali ya mama Samia haitaki mnyanyasike," alisema Homera.

Aliitaka Bodi ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa kushirikiana na viongozi wa kijiji hicho kutoa elimu kwa wananchi kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji vilivyoko kwenye eneo hilo ili visikauke wala kuchafuliwa.

Homera alisema wananchi hao ndiyo walioshika uhai wa chanzo cha Mto Mbaka ambacho kinategemewa na wananchi wa Mji wa Tukuyu, Kyela na baadhi ya kata za Halmashauri ya Busokelo na hivyo wanatakiwa washirikishwe kwenye kukitunza.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Maji ya Ziwa Nyasa, John Kavishe, alisema bodi hiyo iliamua kukihifadhi chanzo hicho kutokana na umuhimu wake kwa wananchi wa Wilaya ya Rungwe pamoja na maeneo mengine ya jirani.

Alisema chanzo hicho kinahudumia zaidi ya wananchi 60,000 wa wilaya hiyo na hivyo walilazimika kukihifadhi liche ya kwamba uhifadhi huo ulikuwa unawaathiri wananchi kwa maeneo yao kutwaliwa.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliishukuru serikali kwa kuwasaidia kumaliza mgogoro huo wakieleza kuwa ulikuwa unawanyima usingizi kutokana na kutojua hatima yao.

Chifu wa Kijiji hicho, Speken Mwakingwe alisema yeye binafsi maeneo yake yaliyokuwa yamechukuliwa yana ukubwa wa ekari saba na ndiyo alikuwa anayategemea kwa ajili ya kuzalisha chakula.

Alisema kwa sasa watakuwa tayari kushirikiana na bodi hiyo itakapokuwa inafanya tathmini ili walipwe fidia huku akiwataka wananchi wake kuwa watulivu.



## HABARI ZANZIBAR

# Dk. Mwinyi awaahidi ushirikiano wanaCCM Kachorora

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaahidi viongozi na wanachama wa CCM tawi la Kachorora ushirikiano katika kukijenga chama kiuchumi na maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na viongozi na wanachama wa maskani hiyo waliofika kujitambulisha na kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar.

Alisema CCM kina mkataba na wananchi ambao ni utekelezwaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM na kueleza kuelekea mwaka 2025 watakua na jukumu la kuwaeleza wananchi hao mambo waliyoyafanya kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake.

Dk. Mwinyi alisema hatua iliyofikiwa ndani ya kipindi cha miaka miwili cha Serikali ya Zanzibar haipo vibaya na matumaini ni makubwa kwa miaka mitano ijayo. Pia aliwahakikishia wananchi na wanachama wa CCM ndani ya kipindi cha miaka mitano miradi mikubwa yote iliyoahidiwa itakamilika.

"Tuna mkataba na wananchi, tunakoelekea mwaka 2025, tutakuwa na jukumu la kusema yapi katika ilani ya uchaguzi tumeyatekeleza, hapo tutakuwa na haki ya kuomba tena kura," alisema.

Aidha, Dk. Mwinyi alisema hatua iliyofikiwa ndani ya kipindi cha miaka miwili cha Serikali ya Zanzibar, awamu ya nane haipo vibaya na yanaonesha matumaini ya miaka mitano ijayo.

Akizungumzia masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia mfuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, Dk. Mwinyi alisema suala hilo pia limetajwa kwenye Ilani ya uchaguzi na kusema kuwa ingawa siyo watu wote watawezeshwa wakati mmoja lakini ni suala linalotekelezwa kwa awamu.

Katibu wa tawi hilo, Said Shabaan Said, alisema wameridhishwa na uongozi wa Dk. Mwinyi wenye kuitekeleza vyema ilani ya uchaguzi ya CCM na muda wote wako tayari kushirikiana na serikali.

## Kusini Pemba watakiwa kushirikiana, kuishauri serikali

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

UONGOZI wa Mkoa wa Kusini Pemba umewataka wananchi wa mkoa huo kuendeleza ushirikiano katika kutekeleza shughuli za maendeleo kwa kutoa maoni na ushauri kwa serikali.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Massoud, aliyasema hayo wakati wa mkutano maalum wa kusikiliza matatizo na kero za wananchi wa Wilaya ya Chakechake.

Alisema kuwa ushirikiano huo unaotolewa na wananchi wa mkoa huo ni chachu ya kutatua baadhi ya kero zinazorudisha nyuma maendeleo.

Alisema utumiaji nguvu na vitisho kwa taasisi zinazohusika na ukusanyaji kodi kwa wafanyabiashara ni jambo ambalo ni kinyume na malengo yaliokusudiwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema bila ya ushirikiano wa wananchi kero hizo na nyingine zingeendelea na kusababisha mivutano isiyo ya lazima kwa wafanyabiashara na taasisi za kodi na kusababisha kuikosesha serikali mapato.

"Ushirikiano wenu na wananchi ndiyo ambayo yametufanya sisi wasimamizi kuona matatizo mbali mbali yaliyomo katika jamii na kuendelea kuzichukulia hatua stahiki, mfano mzuri ni huu wa taasisi zinazohusika na ukusanyaji kodi kwa wafanyabiashara," alisema.

Alisema malalamiko ya wananchi wa mkoa huo yamefanya kuandaa mikutano ambayo inawakutanisha wafanyabiashara na taasisi husika kujadili kasoro hizo kwa maslahi ya taifa.

Alisema kuwa uongozi wa mkoa huo utaendelea kutatua na kuzipatia ufumbuzi changamoto za wananchi ikiwamo kusimamia bei za bidhaa ili zisiendelee kupanda kiholela pamoja na kuweka utaratibu maalum wa upatikanaji wa hati za umiliki wa ardhi kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Chakechake, Abdalla Rashid Ali, alisema kuwa uongozi huo umejipangia utaratibu maalum wa kukutana na wananchi kusikiliza changamoto zinazowakabili.

Naye Ofisa Mdhamini Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Pemba, Ibrahim Saleh Juma, aliwataka wananchi hao kuendelea kuwa wastahimilivu ili kutatua kero za baadhi ya barabara za ndani, pamoja na matengenezo ya Meli ya Mv Mapinduzi 2.

Baadhi ya wananchi waliofika katika kikao hicho walitaja kero zinazowasibu ikiwa ni ubovu wa barabara, huduma za usafiri, ajira pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na wafanyabiashara waagizaji wa vyakula na bidhaa kutoka nje ya nchi, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# 'Kituo cha mafunzo uzalishaji bidhaa kitasaidia vijana kujiajiri'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Taasisi ya Teknolojia ya Karume, Dk. Af-wa Khalfan Mohamed, amesema uanzishwaji wa kituo cha mafunzo ya kitaalamu ya ukuzaji na uzalishaji bidhaa Zanzibar itawasaidia vijana kujiajiri wenyewe na kuipunguzia serikali tatizo la ukosefu wa ajira.

Aliyasema hayo jana kwenye Chuo cha Sayansi na Teknolojia kiliopo Mbweni Zanzibar, baada ya kufungua mafunzo ya siku moja ya kuwasaidia vijana kutumia fursa za uchumi wa digitali kwa kutumia teknolojia.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa kituo hicho kwenye kutafuta njia ya kuwasaida vijana kubadilisha mawazo ya kujiajiri badala ya kutegemea ajira kutoka serikalini.

Alisema kwamba Zanzibar zipo fursa nyingi za kiuchumi ambazo zikitumiwa vizuri na vijana watakuwa na sehemu ya kujiajiri na kucha kusubiri ajira serikalini.

Mratibu wa mradi wa kitaalamu wa ukuzaji na uanzishaji bidhaa, Dk. Khamis Khalid Said alisema lengo la kuanzishwa kwa mradi ni kuwasaidia vijana kupitia Chuo cha Sayansi Karume ambao watapatiwa mafunzo awamu kwa awamu na kujiajiri kupitia fursa za kiuchumi.

Alisema vijana 18 watapatiwa mafunzo kwa kila awamu pamoja na kupatiwa vifaa vya kuanzisha na kuzalisha bidhaa ambazo zinaendena na mazingira ya maeneo waliyopo hasa uchumi wa bahari.

Alisema wanufaika wa mradi huo ni vijana waliomaliza elimu ya lazima pamoja na wanaotaka kuongeza ujuzi kupitia programu za aina mbalimbali kwa kutumia zana zinazopatikana Zanzibar.

Saidi Mussa Khamis kutoka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), alisema matarajio kwa vijana tujikita katika masuala ya uchumi kutoka uchumi wa analogia kwenda digitali kwa kutumia teknolojia zinazopatikana katika visiwa ambazo zitasogeza maendeleo ya vijana hatua kwa hatua.

Baadhi ya vijana akiwamo, Asfat Mohamed na Saleh Ismal walisema mafunzo hayo yatawasaidia kujua utaalamu mpya wa kutafuta fursa za masoko ambayo yapo Zanzibar baada ya kuzalisha bidhaa zao na kupeleka sokoni.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LTD**, Sepco Debt Collection & Auctioneering Co,Ltd tutauza kwa mnada wa hadhara gari iliyoko kwenye jeduali,mnada utafanyika katika yard yetu iliyopo tabata kimanga kuanzia saa tatu asubuhi,Ukaguzi utaanza tu tangazo hili litakapo chapishwa gazetini.

| Aina ya Gari | Namba ya usaji wa gari | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Toyota Harrier | T 994 DSA | 15/02/2023 |

**MASHART YA MNADA**

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 7 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi,Gari inauzwa kama ilivyo

**Mawasiliano piga: -**
**SEPCO - 0715-683777/0769-111174**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**
**(UNDER CAP. 117, R.E. 2002)**

By this deed I, **FOCUNDUS PIRMIN NG'OMA** an adults, **CHRISTIAN** and resident of **MKEKE-MBINGA**, do solemnly state as follows:-

1. That, I hereby absolutely renounce and abandon the use of former name **FAKUNDUS PRIMIN NG'OMA** and in place thereof do assume and adopt the name of **FACUNDUS PIRMIN NG'OMA.**
2. That, in pursuance of such change of name as aforesaid ado hereby declare that, I shall at all material times hereinafter in all records, deed and instruments in writing and in actions, proceedings and transactions and upon all occasion whatsoever use and sign the name of **FOCUNDUS PIRMIN NG'OMA** as the name in place of the former name of **FAKUNDUSPIRMIN NG'OMA.**
3. That, I further authorizes and request all people to designate and address me by such assumed name of **FOCUNDUS PIRMIN NG'OMA.**

I make this declaration consciously believing the name to be in accordance with the provisions of Oaths and statutory Act, 1966.

Signed and Addressed by the said
FOCUNDUS PIRMIN NG'OMA
formally known as
FAKUNDUS PRIMIN NG'OMA



DEPONENT

this 10TH day of January, 2023

BEFORE ME:

NAME : ATIBCUE CRISPO JEMBE

SIGNATURE: ..............................

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEED POLL CHANGE OF NAME**
**(UNDER CAP. 117, R.E. 2002)**

By this deed I, **PASCAL BAKARI MODE** formarly known as **PASKALI MUHODE BAKARI, PASCAL B. MODE** and **PASCAL MHONDE** do hereby absolutely reanounce and abondan the use of my farmer name **PASKALI MUHODE BAKARI, PASCAL B . MODE** and **PASCAL MHONDE** and in lieu thereof to assume as from the date hereof the name of **PASCAL BAKARI MODE**


**AND IN PASUANCE** of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall at all time hereafter in all records deed and instruments in writing and in all action and proceeding and in all dealing and transaction whatsoever use and sign the name of **PASCAL BAKARI MODE**as my name in lieu of the former name of **BASKARI MUHODE BAKARI, PASCAL B. MODE** and **PASCAL MHODE** as renounced due to all transaction's, records, trascript and certificates I prefer to use the name of **PASCAL BAKARI MODE.**

**AND I HERBY AUTHORISED AND REQUEST** all person to designate me by of **PASCAL BAKARI MODE.**

The reason of change name is that the name of **PASCAL BAKARI MODE** has been used on the Identity Card **NIDA** the **PASKALI MUHODE BAKARI** used in Bank **NMB Account Number 22010010746**, and name **PASCAL B. MODE** used in Voter Card, **PASCAL MHODE** used Identity **PPF**, I wish to identified by the real names **PASCAL BAKARI MODE** to be identified.

I the said **PASCAL BAKARI MODE**, make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of the Oaths (Judicial Proceedings) and statutory Decleration Act 1966

**IN WITNESS WHEREOF** I have executed this Deed this **07th day of October, 2021**



## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ENOCH MARWA SANDO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.278 DHA.** AINA YA GARI **TOYOTA KLUGER.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI
**KAH/TR/RB/58/2023**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**EMMANUEL WILSON MWANDETE,** MKAZI WA KIGAMBONI, DAR ES SALAAM. AMEPOTEZA PASSPORT YAKE YA KUSAFIRIA TAREHE 23/01/2023 MAENEO YA KARIAKOO YENYE NAMBA **TAE113670.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DAR/MSI/RB/43115/2023.**


# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Muswada sheria kuwabana wenye nyumba waja

Na Joseph Mwendapole

SERIKALI imesema inakamilisha muswada wa sheria utakaoanzisha chombo cha kusimamia sekta ya milki (Real Estate Regulatory Authority), kwa ajili ya kusimamia na kulinda maslahi ya wapangaji.

Pamoja na shughuli zingine, chombo hicho kitamlazimisha mwenye nyumba kutoza kodi ya mwezi mmoja mmoja badala ya utaratibu wa sasa ambao huamua kupokea kodi ya kuanzia miezi sita hadi mwaka mmoja.

Hayo yalisemwa juzi Dar es Salaam na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, wakati akifungua mafunzo ya wiki moja kwa mawakala wa mali zisizohamishika. Mafunzo hayo yanaendeshwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na bada ya muda yatakuwa yakifanyika kwa mwaka mmoja.

Waziri alisema kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu wenye nyumba kuwalazimisha kulipa kodi ya miezi sita au mwaka mmoja, hivyo sheria hiyo itasaidia kusimamia maelekezo ya serikali. Aliipongeza CBE kwa kuanzisha kozi hiyo aliyosema imekuja wakati mwafaka.

"Sheria hii italazimisha mwenye nyumba kupokea kodi ya mwezi mmoja mmoja lakini itaweka nafasi ya majadiliano baina ya mpangaji na mwenye nyumba na wakizungumza wakikubaliana kulipa mwaka au miezi sita kwa hiari hiyo inaruhusiwa lakini haipaswi kuwa lazima," alisema.

Dk. Mabula aliwataka mawakala nao kuzingatia maadili ili kuifanya kazi hiyo kuwa na heshima kama ilivyo kwa nchi nyingi za Afrika Mashariki kwa kuwa uzoefu unaonyesha kwamba madalali wengi wamekuwa wakifanya holela kazi hiyo.

Alisema baadhi ya madalali wamekuwa na kawaida ya kupandisha gharama za nyumba na vyumba vya kupangisha kwa lengo la kupata kamisheni kubwa hali ambayo inaumiza wananchi wengi hasa wenye uwezo mdogo.

"Unakuta nyumba inapangishwa kwa Sh. 100,000 kwa mwezi lakini dalali anamwambia mpangaji kwamba inapangishwa kwa Sh. 200,000. Sasa mpangaji akijiongeza akaenda kwa mwenye nyumba akaambiwa kwamba inapangishwa kwa Sh. 100,000 heshima yako na uaminifu wako unapotea," alisema Dk. Mabula.

Alisema baadhi yao wamekuwa wakiuza mali ambazo hawajaambiwa kuuza kama viwanja na nyumba hali ambayo imesababisha migogoro mingi huku wakitoweka kusikojulikana na kusababisha wanunuzi kubaki wakihangaika.

"Ndiyo maana nasisitiza kwenye mafunzo haya mwafundishe maadili. Ukiwa na maadili watu watakuwa mabalozi wako kwamba ukitaka kazi hii ifanikiwe mwone fulani lakini kama ni tapeli hutapata kazi na utaishia kutafutwa kwa wizi," alisema Waziri Mabula.

## IGP ataka WCF kuwajengea uelewa polisi utendaji wa kazi

Na Maulid Mmbaga

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura (pichana), amewataka watendaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kuwajengea uelewa askari polisi wa mikoa katika kuelewa majukumu yao na ya taasisi hiyo.

Akizungumza jana mkoani Kilimanjaro wakati akifungua kikao kazi cha siku mbili, IGP Wambura aliwasisitiza makamanda wa polisi kudumisha uhusiano na ushirikiano kati yao na WCF.

Wambura alisema anaamini taasisi hiyo itaitumia nafasi hiyo vizuri kuwaelimisha makamanda ili waelewe WCF ni nini, majukumu yake ni yapi, wao wana majukumu yapi na wajibu wao ni nini wanapokwenda kufanya kazi pamoja.

"Nategemea yale yote mtakayoyapata kutokana na mawasilisho yatakayotolewa mtayasikiliza kwa makini. Tumieni muda wenu myaelewe vizuri ili wale wote mnaowaongoza wafahamu WCF ni kitu gani na wanapokutana kikazi wajue wanawajibika vipi," alisisitiza Wambura.



Aliongeza kuwa elimu hiyo ni kwa ajili ya kuongeza ufahamu ili kuingia kwenye utendaji ambao ni mzuri na wenye tija na wanaoutazamia usiwe na mivutano, mikwaruzano na ucheleweshaji wa kazi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema ili kutekeleza jukumu la kulipa fidia kwa ufanisi, pamoja na kuwekeza kwenye miundombinu na kuwa na rasilimali watu wenye weledi, taasisi hiyo imewekeza katika kujenga uhusiano na ushirikiano na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisema ushirikiano huo umewawezesha kubadilishana uzoefu, taarifa na kutekeleza baadhi ya majukumu pamoja na kwamba jeshi hilo ni moja ya wadau wa kimkakati kwao.

"Ili WCF iweze kulipa fidia za ajali zinazotokea barabarani na zenye viashiria vya kijinai, sheria inawataka kuwe na ripoti ya polisi kama uthibitisho," alisema Mduma.


www.nbc.co.tz

NBC Benki ya Taifa ya Biashara Daima Karibu Nawe.

TAARIFA KWA UMMA

MABADILIKO YA GHARAMA ZA HUDUMA ZA BENKI

Mpendwa mteja, Uongozi wa benki ya NBC unapenda kukufahamisha kwamba kutakuwa na mabadiliko ya gharama za kibenki kuanzia tarehe 3 Machi 2023. Gharama nyingine ambazo hazijaoneshwa hapa chini hazitabadilika.

| SERVICE NAME | NEW CHARGES | | | |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | EUR | GBP |
| **Alternative Channels** Bill Payment Mobile Channels | Free | N/A | | |
| **Alternative Channels** Mobile Banking Fund Transfer - NBC to NBC | 1000 | 1 | N/A | |
| **Alternative Channels** * BIR Funds Transfer to Mobile Wallets | 0 - 9,999 = 1,000<br>10,000 - 49,999 = 3,500<br>50,000 - 99,999 = 4,800<br>100,000 - 299,999 = 6,300<br>300,000 - 1,500,000 = 10,800 | N/A | | |
| **Alternative Channels** * Mobile Banking Fund Transfer - NBC to Non-NBC | 11,800 | 5 | N/A | |
| **Mobile Banking only** Balance Enquiry | 500 | N/A | | |
| **NBC ATM** Cash withdrawal for Shambani Individual | 1,000 | N/A | | |
| **NBC ATM** Balance enquiry for Shambani Individual | 400 | N/A | | |
| **International ATM** Shambani Individual - Balance enquiry | 1,500 | N/A | | |
| **Quarterly Debit Card Fee** Private Banking / La Riba Private Banking /Privilege Banking | 12,500 | 6 | N/A | |
| **Quarterly Debit Card Fee** Kua Nasi, Shambani, Student | 3,000 | N/A | | |
| **Quarterly Debit Card Fee** Corporate Card | 20,000 | N/A | | |
| **Quarterly Debit Card Fee** All other products | 5,000 | 6 | N/A | |
| **Card Replacement / Re-issuance** Lost Platinum card (Privilege / Private / La Riba/Corporate) | 30,000 | 15 | N/A | |
| **Agency Banking** Debit card linkage fee via POS | 4,000 | N/A | | |
| **Opening Account Balance** Privilege Banking /La Riba privilege Banking | 10,000 | 5 | | |
| **Cash Withdrawal Fee over the counter** Kua Nasi product | Below 1M = 2,000<br>Above 1M = 4,000 | N/A | | |
| **Maintenance Fee** Fasta Akaunti | 800 | N/A | | |

Bei zote zimejumlishwa na kodi ya ongezeko la thamani (VAT).
Huduma zenye alama * zimejumuisha tozo za serikali.
Wasiliana nasi 0800 711 177 (BURE) au contact.centre@nbc.co.tz

# KOCHA BARES APEWA MTIHANI MGUMU PRISONS LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Timu ya Tanzania Prisons, umempa mtihani mgumu Kocha Mkuu mpya, Mohammed Abdallah 'Bares', baada ya kumtaka kuipandisha hadi nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tanzania Prisons inashika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo, baada ya kushinda michezo mitano, sare sita na kupoteza 10, hivyo kujikusanyia pointi 21sawa na Dodoma Jiji FC iliyoko nafasi ya 13, wakati huu zikiwa zimebakiza mechi tisa kabla ya msimu huu wa 2022/23 kumalizika.

Katika michezo hiyo tisa uongozi huo umepanga kukusanya alama 27 kwa kutafuta pointi tatu muhimu katika kila mchezo uliopo mbele yao ikiwamo mechi yao ijayo dhidi ya Mtibwa Sugar itakayopigwa Ijumaa hii katika uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Tanzania Prisons, Enock Manguku, alisema tayari Bares ameshaanza kazi ya kukinoa kikosi chao na kukubaliana na mikakati yao ya kuhakikisha wanapambana kutafuta pointi tatu katika michezo tisa iliyobaki.**

Alisema wanatambua ligi imekuwa na ushindani mkubwa na itakuwa ngumu kupata pointi zote 27 katika michezo iliyobaki, ila cha muhimu wanahitaji kumaliza msimu timu hiyo ikiwa nafasi ya saba kwenye msimamo.

"Bares amekubaliana na mipango yetu ambayo haina tofauti kubwa na malengo yake, ameshaanza kazi na mechi yake ya kwanza kuwapo kwenye benchi itakuwa hapa nyumbani dhidi ya Mtibwa Sugar kuhakikisha tunabakiza pointi tatu.

"Tunaimani na kocha huyo, anaweza kutufikisha katika malengo yetu ya kupata pointi kila mechi kama si zote 27 basi hata nusu yake ili tuondoke hapa chini (nafasi ya 12) na kupanda hadi nafasi ya saba," alisema Manguku.

Kwa upande wa Bares, alisema anafahamu malengo na mkakati aliyopewa na viongozi, hivyo anapambana kwa uwezo wa Mungu kufikia malengo hayo ya kuiondoa timu nafasi ya chini kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Alisema kibarua kigumu alicho nacho ni kufanyia kazi madhaifu yao na kuboresha kwenye ubora zaidi ili kufikia malengo yao ya kutafuta pointi kila mechi iliyopo mbele yao.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, natambua tuko nafasi ambayo si nzuri na usipokuwa makini kutafuta matokeo unaweza kushuka, umakini unaotakiwa ni kutafuta pointi kila mechi ili kufikia kile kinachotarajiwa na viongozi kuondoka huku chini kwenye presha ya kushuka na kupanda juu katika nafasi ambazo tutakuwa salama," alisema Bares mabaye hiyo itakuwa mechi yake ya kwanza tangu ajiunge na miamba hiyo ya Mbeya.

**WANAMITINDO...**




Wanamitindo wakichuana vikali katika Ukumbi wa Warehouse Arena, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni maandalizi kuelekea maadhimisho ya miaka 20 ya maonyesho ya ubunifu wa mavazi yajulikanayo Lady In Red, yanayotarajiwa kufanyika Februari 11, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Sauti za Busara kurindima siku 3 Z'bar*

**Na Moshi Lusonzo**

TAMASHA la Muziki la Kimataifa la Sauti za Busara linatarajiwa kutikisa visiwani Zanzibar wiki ijayo, kwa kuwakutanisha wasanii nyota zaidi ya 30 kutoka sehemu mbalimbali duniani, imeelezwa.

Akizungumza katika uzinduzi wa tamasha hilo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Sauti za Busara, Yusuf Mahmoud, alisema litafanyika katika eneo la Ngome Kongwe kwa muda wa siku tatu kuanzia Februari 10, mwaka huu.

Mahmoud alisema mwaka huu tamasha hilo ambalo limepata umaarufu duniani kote, litakuwa tofauti kwa kuwa litakuwa likitimiza miaka 20 tangu kuanzishwa kwake.

Alisema katika tamasha la mwaka huu, burudani zitatolewa na bendi mbalimbali kutoka Bara la Afrika, Marekani, Asia na wanamuziki nyota wa taarabu na singeli kutoka Tanzania.

Mkurugenzi huyo amewataja wasanii kama Patricia Hilal na Mzee wa Bwax kuwa watapata nafasi ya kutumbuiza katika jukwaa moja.

Aliwataja wasanii wengine watakaotumbuiza kuwa ni Tiken Jah Fakoly kutoka Ivory Coast, BCUC (Afrika Kusini), Zawoze (Reunion), Ston Town Rockers, Diamian Soul wote kutoka Tanzania. Pia wasanii wengine ni Culture Music Taarab, Uwaridi Female Band, Zan Ubuntu na Zenj Boy kutoka Zanzibar Zily (Mayote), Naxx (DRC), Atse Tewodros (Ethiopia), Sana Cissokho (Senegal), Majestad Negre (Petro Rica), Obert Dube (Zimbabwe) na Kloubadya (Reunion).

"Hatua tuliyofikia ni ushahidi kwamba wasanii wengi wakubwa kwa kutumia jukwaa letu wametambulika na kuitwa sehemu mbalimbali duniani. Mwaka huu watapata nafasi nyingine ya kukuza majina yao na ndivyo tunavyofanya kila siku," alisema Mahmoud.

Aidha, alisema tamasha hilo litabeba ujumbe maalum unaosema 'Tofauti zetu, utajiri wetu', ambao unahimiza wasanii kutumia muziki kutoka mataifa tofauti na kuuweka pamoja kwa ajili ya manufaa ya wengi.

## Yanga Princess, JKT Queens vitani

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya sita ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea leo kwenye viwanja mbalimbali nchini, lakini macho na masikio ya mashabiki yatakuwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam wakati vinara wa ligi hiyo, JKT Queens watakapowakaribisha Yanga Princess kwenye mechi inayotarajiwa kuwa kali na ya kusisimua.

Maafande wa JKT Queens ambao msimu huu wanaonekana wana kikosi bora na wanausaka ubingwa kwa udi na uvumba, wanakwenda kucheza mechi hiyo wakiwa hawajapoteza hata moja kati ya sita walizocheza hadi sasa, wakishinda tano na kutoka sare moja tu, hivyo kuwa kileleni na pointi zao 16.

Yanga Princess ambayo inashika nafasi ya nne ikiwa na alama 13, nayo baadhi ya viongozi wao wamekaririwa wakisema msimu huu iwe usiwe wanautaka ubingwa wa soka kwa wanawake, hivyo wanatakiwa kushinda mechi hiyo ili kuwa sawa kwa pointi na JKT Queens, kwani kinyume cha matokeo hayo, bado watakuwa mbali na azma yao hiyo.

## Zimamoto bado yauona ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya Timu ya Zimamoto kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Uhamiaji juzi, imesema bado inasafari ya kusaka matokeo zaidi iwapo wanautaka ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohmed Ali Hilali, alisema bado wanahitaji kupata matokeo katika michezo iliyosalia ili kuhakikisha wanashinda taji la Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema bado hajakata tamaa ya kuubeba ubingwa huo licha ya ligi hiyo kuzidi kuwa ngumu kuliko alivyotarajia hapo awali alipoanza safari ya mzunguko huu wa lala salama.

Hilali alisema iwapo timu hiyo itashinda michezo mitano mfululizo katika mzunguko huu atakuwa na imani kubwa ya kuendelea na mbio za ubingwa na endapo wakipoteza michezo hiyo basi matumaini yake atawekeza katika kushinda Kombe la FA.

"Sisemi kama nimepoteza matumaini ya ubingwa bado ninayo, lakini nitakuwa nayo zaidi pale nitakaposhinda michezo mitano mfululizo hususan ambayo nitacheza na vinara wa ligi hii, lakini vinginevyo nitajiweka katika mbio za Kombe la FA," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ENZO SAFI CHELSEA

KLABU ya Chelsea wameweka dau la euro 120 kumnunua kiungo wa kati wa Benfica na Argentina, Enzo Fernandez, katika hatua ambayo itamfanya kuvunja rekodi ya usajili ya England. ***(Mail)***

### BELLERIN KUMRITHI PORRO

KLABU ya Sporting Lisbon itachukua nafasi ya Porro na kumchukua beki mwenzake wa kulia wa Uhispania, Hector Bellerin mwenye miaka 27, kutoka Barcelona. ***(Fabrizio Romano)***

### OFA KIBAO KWA ELANGA

KLABU ya Manchester United imepokea ofa 10 za mkopo kwa winga Anthony Elanga, huku Borussia Dortmund na PSV Eindhoven zikiwa miongoni mwa klabu zinazomtaka, lakini kocha Erik ten Hag anasita kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kuondoka. ***(Fourfour Two)***

### SPENCE KUONDOKA SPURS

BEKI wa pembeni wa Tottenham, Djed Spence mwenye umri wa miaka 22, anatarajiwa kuondoka kwa mkopo katika Klabu ya Rennes ya Ufaransa kwa muda wote uliosalia. ***(BBB Sport)***

### TRAORE ANUKIA KUHAMA

KLABU ya Bournemouth inakaribia kukubaliana ada na Sassuolo ya Serie A kwa ajili ya kiungo wao wa Ivory Coast, Hamed Traore, mwenye miaka 22. ***(90min).***

### YOURI KUTUA ARSENAL

ARSENAL pia wanafikiria kuwasilisha ombi la kuchelewa kwa kiungo wa Leicester, Youri Tielemans. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 25, mkataba wake unamalizika majira joto msimu huu.***(90 Minutes)***

### MAGUIRE AIKATALIA UNITED

NAHODHA wa Manchester United Harry Maguire mwenye miaka 29, amekataa mpango wa mkopo kutoka kwa Inter Milan ili kupigania nafasi yake Old Trafford - lakini atatathmini upya msimamo wake msimu wa majira ya joto. ***(Daily Star)***

### PORRO ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham imekaribia kukamilisha dili la kumsaini beki wa kulia wa Uhispania, Pedro Porro mwenye miaka 23, kwa euro milioni 45 kutoka Sporting Lisbon. ***(Telegraph)***

### KANTE NA LIVERPOOL

LIVERPOOL imaweza kufanya hatua ya kushtukiza ili kuimarisha safu yao ya kiungo kwa kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante mwenye miaka 31, ambaye mkataba wake unamalizika Stamford Bridge msimu huu wa majira ya joto. ***(El Nacional)***

### BENFICA NA KIKWAZO

KLABU ya Benfica hapo awali waliishutumu Chelsea kwa kujaribu kumvuruga Enzo Fernandez, huku kocha wa timu hiyo ya Ureno, Roger Schmidt, akitangaza kuwa mbio zao "zimefungwa". ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JORGINHO ATAJWA KUNUKIA ARSENAL

**LONDON,** England

**Tielemans wa Leicester naye yumo ni baada ya kumkosa Caicedo wa Brighton...**

KLABU ya Arsenal bado wana nia ya kuongeza sura mpya katika safu yake ya kati na inasemekana watacheza dakika za mwisho kwa Jorginho wa Chelsea na Youri Tielemans wa Leicester City kabla ya saa ya mwisho jana usiku.

**Tielemans ni mmoja wa mastaa wakubwa wa Leicester, akitokea katika mechi zote 20 za Ligi Kuu msimu huu huku akichangia mabao matatu na asisti katika mechi 18 alizoanza.**

Jorginho yuko katika msimu wake wa tano Stamford Bridge na anasalia kuwa sehemu muhimu ya kikosi cha Chelsea, ameanza ligi mara 15 msimu huu, ikiwa ni pamoja na kuvaa kitambaa cha unahodha katika mechi zao mbili za hivi majuzi.

Hata hivyo, wachezaji wote wawili wako katika miezi sita ya mwisho ya mikataba yao na wanatazamiwa kupatikana kupitia uhamisho wa bure mwisho wa kampeni msimu huu, na klabu zao zinaweza kuwa tayari kukubali punguzo kubwa la ada ya uhamisho.

Kwa mujibu wa Daily Mail harakati za Arsenal kumtafuta nyota wa Brighton na Hove Albion, Moises Caicedo, mwenye umri wa miaka 21, zinaonekana kutofaulu na sasa wanamwona Jorginho kama mbadala anayekubalika.

Ripoti hiyo inasema Chelsea wako tayari kumruhusu mchezaji huyo wa Kimataifa wa Italia kuondoka, ikionyesha kuwa hatatumika kama ujio wa Enzo Fernandez wa Benfica utatimia.

Pia Arsenal watafanya msukumo mwingine kwa Caicedo na Martin Zubimendi wa Real Sociedad, lakini wanachukuliwa kuwa chaguo lisilowezekana.

Wakati huo huo, 90min inadai Leicester ingekuwa wazi zaidi kuruhusu Tielemans kuondoka ikiwa hawakufungwa kwenye vita vya kushuka daraja, lakini kwa hali ilivyo watahitaji ada kubwa ya uhamisho badala ya kusalimika kwao Ligi kuu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,072,5

JACKPOT
MECHI WIKI HII

TAREHE: 01,02 NA 03 FEBRUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/02/23 | 22:00 | Waalwick vs GO Ahead Eagles | 2.30 | 3.37 | 2.87 |
| 02. 01/02/23 | 22:15 | Grasshoppers vs FC Basel | 2.79 | 3.31 | 2.27 |
| 03. 01/02/23 | 22:45 | Oxford Utd vs Barnsley | 2.49 | 3.34 | 2.64 |
| 04. 01/02/23 | 22:45 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.21 | 3.29 | 3.14 |
| 05. 02/02/23 | 02:00 | Tlaxcala FC vs Alebrijes De Oaxaca | 2.52 | 3.01 | 2.70 |
| 06. 02/02/23 | 06:05 | Club Atletico La Paz vs Cimarrones De Sonora | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 07. 02/02/23 | 17:00 | Kayserispor vs Basaksehir | 2.70 | 3.39 | 2.44 |
| 08. 02/02/23 | 17:00 | Chennaiyin FC vs Delhi Dynamos FC | 2.40 | 3.42 | 2.56 |
| 09. 02/02/23 | 20:00 | Adana Demirspor vs Fenerbahce | 2.92 | 3.51 | 2.23 |
| 10. 02/02/23 | 20:00 | Anorthosis Famagusta vs Omonia Nicosia | 2.76 | 3.24 | 2.51 |
| 11. 02/02/23 | 22:45 | Zulte Waregem vs Mechelen | 2.63 | 3.42 | 2.42 |
| 12. 03/02/23 | 06:00 | San Luis vs Puebla FC | 2.32 | 3.19 | 3.03 |
| 13. 03/02/23 | 14:00 | Tiddim Road Athletic Club vs Mohammedan SC | 2.39 | 3.28 | 2.65 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money


SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AGUERO ATAKA HAALAND AUNGWE MKONO CITY




**MANCHESTER,** England

SERGIO Aguero amesema Erling Haaland anahitaji uungwaji mkono kutoka kwa wachezaji wenzake wa Manchester City ili kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu England huku akiamini kuwa ni Lionel Messi pekee ndiye anayeweza kubeba timu kwa heshima kubwa peke yake.

Haaland alifikisha mabao 25 kwa msimu wa Ligi Kuu kwa kufunga hat-trick City ilipoizaba Wolves 3-0 katika mechi yao ya hivi majuzi kwenye kinyang'anyiro hicho.

Licha ya ushujaa wa Haaland, kikosi cha Pep Guardiola kinawafuata vinara wa ligi Arsenal kwa pointi tano baada ya kucheza mchezo mmoja zaidi, na nyota wa zamani City, Aguero amesema mshambuliaji huyo hawezi kufanya hivyo peke yake.

Alipoulizwa kama Haaland anaweza kuhamasisha City kunyakua taji la tano la ligi katika misimu sita, Aguero aliiambia Stake.com: "Itabidi tuone hilo bado. Bado kuna mengi ya msimu ujao. Haaland, ambaye amekuwa akikusanya namba ambazo zitavunja rekodi za kihistoria, atachukua sehemu kubwa katika hilo."

Aguero alisema kuwa kwa vyovyote vile, isipokuwa Messi, hakuna mchezaji mmoja ambaye anaweza kushinda ligi peke yake, kwani inahusu timu, na City wana orodha ya wachezaji wenye vipaji na wafanyakazi wa kipekee. Wametoa ushahidi mwingi wa kimo chao, na unajua watapambana hadi mwisho.



# Ziyech mambo safi PSG

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Chelsea, Hakim Ziyech, anaripotiwa kukaribia kujiunga na PSG, huku mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yakiendelea.

Kwa mjibu wa Foot Mercato, Ziyech alitarajiwa kumaliza kibarua chake na Chelsea kabla ya dirisha dogo la Januari kufungwa usiku wa jana Jumanne.

'The Blues' wanajadili mkataba wa mkopo wa mchezaji huyo wa Morocco na Paris Saint-Germain.

Na mchezaji huyo amekataa ofa za Newcastle United na Everton, kwani anataka kujiunga na PSG.

Ziyech ameona maendeleo yake yakidumaa tangu ajiunge na Chelsea kutoka Ajax Julai 2020.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, aliwasili Stamford Bridge kama mchezaji bora wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie.

Lakini masuala ya utimamu wa mwili na hali duni vimemsumbua katika kipindi cha miaka miwili na nusu iliyopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco amecheza kwa dakika 610 pekee, akianza mechi sita.

Na baada ya kiwango kizuri kwenye Kombe la Dunia 2022, mchezaji huyo amekuwa na hamu ya kuondoka Chelsea.

## HABARI MICHEZO

549,524/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/02/23 | 18:00 | Preston North End vs Bristol City | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 02. 04/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Queens Park Rangers | 3.00 | 3.20 | 2.39 |
| 03. 04/02/23 | 18:00 | Reading FC vs Watford FC | 2.70 | 3.20 | 2.60 |
| 04. 04/02/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KVC Westerlo | 2.75 | 3.45 | 2.41 |
| 05. 04/02/23 | 22:00 | FC Emmen vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 04/02/23 | 23:00 | Excelsior Rotterdam vs RKC Waalwijk | 2.70 | 3.35 | 2.49 |
| 07. 04/02/23 | 23:00 | Stade Rennes vs Lille OSC | 2.30 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 04/02/23 | 23:30 | Estoril Praia vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 09. 05/02/23 | 03:30 | Atletico Lanus vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.31 | 2.85 | 2.80 |
| 10. 05/02/23 | 03:30 | Argentinos Juniors vs Racing Club Avellaneda | 2.60 | 2.70 | 2.60 |
| 11. 05/02/23 | 15:30 | Royal Antwerp FC vs Club Brugge | 2.49 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 05/02/23 | 16:00 | Villarreal CF B vs Granada CF | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 13. 05/02/23 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.49 | 3.15 | 2.37 |
| 14. 05/02/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs NEC Nijmegen | 2.40 | 3.35 | 2.85 |
| 15. 05/02/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Leeds United | 2.60 | 3.30 | 2.60 |
| 16. 05/02/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs FC Nantes | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 17. 05/02/23 | 17:00 | Torino FC vs Udinese Calcio | 2.24 | 3.20 | 3.25 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 01/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4518 | Real Kashmir vs Aizawl FC | 2.33 | 3.01 | 2.95 |
| 15:35 | 5429 | Alshoulla vs Hajer Club | 2.82 | 2.76 | 2.61 |
| 15:45 | 5507 | AL Arabi (SA) vs AL Qaisoma | 1.72 | 3.10 | 4.20 |
| 15:50 | 5298 | AL Hazm vs Al Orubah | 1.68 | 3.36 | 4.86 |
| 16:30 | 2625 | Kenkre FC vs Minerva FC | 6.40 | 3.97 | 1.44 |
| 16:35 | 2641 | AL Sahel vs Al Salmiyah | 3.40 | 3.25 | 1.87 |
| 17:00 | 2901 | Kasimpasa vs Giresunspor | 2.02 | 3.50 | 3.39 |
| 17:00 | 3748 | Ceske Budejovice vs Hradec Kralove | 2.74 | 3.31 | 2.31 |
| 17:00 | 4308 | Gaziantep BB vs Hatayspor | 2.04 | 3.45 | 3.40 |
| 20:00 | 1459 | Galatasaray vs Umraniyespor | 1.23 | 5.95 | 10.42 |
| 20:00 | 1724 | Calcio Lecco vs Albinoleffe | 2.54 | 3.15 | 2.78 |
| 20:00 | 2752 | Trabzonspor vs Antalyaspor | 1.68 | 3.71 | 4.78 |
| 20:00 | 3256 | Feralpisalo vs Padova | 2.09 | 3.14 | 3.67 |
| 20:00 | 3964 | Fiorentina vs Torino | 2.03 | 3.23 | 3.65 |
| 20:00 | 4994 | Vicenza vs Novara | 2.07 | 3.35 | 3.46 |
| 20:00 | 5038 | RB Leipzig vs Hoffenheim | 1.55 | 4.40 | 5.37 |
| 20:00 | 5158 | Pro Vercelli vs Pro Patria | 2.31 | 3.09 | 3.19 |
| 20:30 | 4345 | Paksi FC vs Ferencvaros TC | 4.37 | 4.06 | 1.60 |
| 20:45 | 1049 | Eupen vs Racing Genk | 5.00 | 4.20 | 1.57 |
| 21:00 | 1025 | Reims vs Lorient | 1.81 | 3.53 | 4.18 |
| 21:00 | 1509 | Lille vs Clermont Foot | 1.47 | 4.30 | 6.19 |
| 21:00 | 1679 | Miedz Legnica vs Lech Poznan | 4.37 | 3.43 | 1.73 |
| 21:00 | 2841 | Toulouse vs Troyes | 1.74 | 3.87 | 4.16 |
| 21:00 | 3235 | Angers vs AC Ajaccio | 2.24 | 3.13 | 3.23 |
| 21:00 | 4264 | Nantes vs Marseille | 4.38 | 3.63 | 1.75 |
| 22:00 | 1063 | Maritimo vs Porto | 10.94 | 5.57 | 1.24 |
| 22:00 | 2026 | Al Ahly Cairo vs Auckland City | 1.30 | 4.86 | 7.86 |
| 22:00 | 5628 | Waalwick vs GO Ahead Eagles | 2.25 | 3.41 | 2.92 |
| 22:15 | 2806 | Grasshoppers vs FC Basel | 2.96 | 3.32 | 2.17 |
| 22:45 | 1259 | Aberdeen vs St Mirren | 2.00 | 3.33 | 3.63 |
| 22:45 | 1284 | Motherwell vs St Johnstone | 2.08 | 3.23 | 3.53 |
| 22:45 | 2463 | Oxford Utd vs Barnsley | 2.49 | 3.34 | 2.64 |
| 22:45 | 2519 | Kingstonian vs Margate | 2.37 | 3.35 | 2.63 |
| 22:45 | 2825 | Union Saint Gilloise vs Royal Antwerp | 2.08 | 3.42 | 3.21 |
| 22:45 | 2859 | Celtic vs Livingston | 1.10 | 8.98 | 18.96 |
| 22:45 | 3093 | Hearts vs Rangers | 4.97 | 4.28 | 1.56 |
| 22:45 | 3219 | Mainz vs Bayern Munchen | 5.56 | 4.71 | 1.50 |
| 22:45 | 3843 | Yate Town vs Hendon | 2.47 | 3.63 | 2.39 |
| 22:45 | 4912 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.35 | 3.18 | 2.98 |
| 23:00 | 1003 | Montpellier vs Paris St Germain | 7.71 | 5.14 | 1.33 |
| 23:00 | 1107 | Juve Stabia vs Crotone | 3.51 | 3.14 | 2.14 |
| 23:00 | 1580 | AD Grecia vs CS Herediano | 3.32 | 3.32 | 2.01 |
| 23:00 | 1588 | Monaco vs AJ Auxerre | 1.30 | 5.38 | 8.17 |
| 23:00 | 1762 | Lyon vs Brest | 1.50 | 4.29 | 5.78 |
| 23:00 | 4718 | Lens vs Nice | 1.71 | 3.49 | 4.88 |
| 23:00 | 5554 | Manchester Utd vs Nottingham | 1.46 | 4.31 | 6.36 |
| 23:00 | 5606 | Betis vs Barcelona | 4.59 | 3.72 | 1.71 |
| 23:00 | 5657 | Real Madrid W vs Real Sociedad W | 1.51 | 4.05 | 5.19 |
| 23:00 | 5743 | Roma vs Cremonese | 1.43 | 4.33 | 6.98 |
| 23:00 | 5905 | Rennes vs Strasbourg | 1.54 | 3.99 | 5.78 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA SC WATAKIWA UMOJA, SINGIDA BS IKIWATISHIA NYAU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wanachama na mashabiki wa Simba wakitakiwa kuwa wamoja baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, Klabu ya Singida Big Stars imeahidi kutonesha vidonda kabla havijapona kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Ijumaa ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema jana kuwa, baada ya uchaguzi kumalizika wanachama na mashabiki wa Simba wanatakiwa kuungana kwa ajili ya kuipeleka klabu mbele kwa sababu ndiyo lengo lao mama.**

'Uchaguzi huwa unaacha makundi, lipo kundi ambalo mgombea wake ameshinda linashangilia, lakini lipo ambalo mgombea wake hajapata kura za kutosha, wanabaki na makovu, lakini wote tulikuwa tunapambana kuiongoza Simba, lengo ni kuja kuisaidia, bahati tu mbaya mmoja hajapata.

"Uchaguzi sasa umekwisha waliopatikana wamepatikana, wote tuliobaki tunatakiwa kuungana kwa pamoja kuwasaidia viongozi walioshinda kwa sababu lengo letu ni klabu isonge mbele, tukiwadhohofisha maana yake tumeidhohofisha Simba, niwaombe tu Wanasimba kuwa wa wazi adui yetu ni timu zilizo kwenye Ligi Kuu na michuano mingine ya ndani na ya kimataifa," alisema Ahmed.

Jumapili iliyopita, klabu hiyo kubwa na kongwe nchini ilifanya uchaguzi wake ambapo aliyekuwa Mwenyekiti kabla ya uchaguzi, Murtaza Mangungu, alichaguliwa tena kuiongoza klabu hiyo kwa miaka minne, huku Wajumbe wa Bodi waliochaguliwa ni Dk. Seif Ramadhani Muba, Asha Baraka, CPA Issa Masoud, Dk. Rodney Chiduo na Selemani Haroub.

Wakati Simba ikisema hayo, kikosi cha Singida Big Stars kipo jijini Dar es Saalam kwa ajili ya kuikabili timu hiyo Ijumaa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku kikiapa kile ilichosema kuwa ni vidonda na si makovu kwa sababu muda ni mfupi sana watakaokutana nao baada ya uchaguzi.

Ofisa Mtendaji Msaidizi wa Klabu hiyo, Muhibu Kanu, alisema hawajaja Dar es Salaam kushangaa maghorofa, badala yake wametumwa pointi tatu na wakazi wa Mkoa wa Singida.

"Simba ni timu kubwa imefanya mengi makubwa ndani na nje ya nchi, lakini sisi tumejipanga kupata matokeo mazuri kwenye mechi hiyo na wachezaji wetu wapo vizuri kasoro kipa wetu, Khomein Aboubakar anayesumbuliwa na majeraha, lakini waliobaki wote wako vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kwenye mechi yetu hiyo.

"Tuwaambie tumekuja Dar es Salaam kuhakikisha tunapata pointi tatu, tunajua sehemu gani tuwashike ili kupata pointi tatu," alisema Muhibu.

Kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Novemba 9, mwaka jana, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Liti mkoani Singida.

## Haier yaipa nguvu mpya Yanga CAF

INATOKA UKURASA 24

taba na kampuni hiyo kubwa duniani.

"Young Africans SC imeingia mkataba na Kampuni ya Haier wenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 kama mdhamini mkuu wa Kombe la Shirikisho barani Afrika," alisema Hersi.

Naye mwakilishi wa Haier, Leon Chi, amesema wamevutiwa kufanya kazi na Yanga kwa sababu ndio klabu yenye mafanikio zaidi hapa Tanzania, ikitwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara 28, mataji mawili ya Kombe la Shirikisho la Azam na makombe sita ya Ngao ya Jamii, lakini imefanikiwa kutengeneza rekodi kubwa ya kutokupoteza (Unbeaten).

"Hatupo Tazania kwa ajili ya biashara tu bali pia kusaidia jamii kubwa ya vijana wenye vipaji kupitia mchezo wa mpira wa miguu. Tunafuraha kubwa kushirikiana na timu hii iliyopata ushindi wa kihistoria nchini Tunisia dhidi ya Club Africain.




## Baleke aiwahi Singida BS

INATOKA UKURASA 24

masomo yake na kesho (leo), atakuwapo mazoezi akiendelea na majukumu yake ya kukinoa kikosi chetu kuelekea michezo iliyopo mbele yetu, tukianza na Singida Big Stars," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine Ofisa Mtendaji Mkuu Mpya wa Simba, Imani Kajula, leo anatarajia kukutana na mtangulizi wake, Barbara Gonzalez kujadiliana mambo mbalimbali kwa lengo la kuiwezesha klabu hiyo kupiga hatua.

Alisema wanakutana kwa ajili ya kupeana mikakati ya kuelekea michezo ya kimataifa wanayotarajiwa kuanza rasmi Februari 11, mwaka huu ugenini nchini Guinea dhidi ya Horoya AC.

"Mipango yangu ni kuona Simba inakuwa bora kwa vitendo, kuna mambo mengi ya kufanya ikiwamo kujiimarisha zaidi kuelekea michezo yetu ya kimataifa tunaenda kucheza dhidi ya Horoya AC ya Guinea.

"Tunahitaji kufanya vizuri mchezo huu wa ugenini na kesho (leo), tunakutana na Barbara kuzungumza mambo mbalimbali na kuweka mipango mizuri kuelekea mchezo huo na iliyopo mbele yetu," alisema Kajula.

# Michezo

Jumatano Februari 1, 2023

Nipashe




Jorginho atajwa Arsenal UKURASA 21

UZI WA CAF...



Kutoka kushoto ni Makamu wa Rais wa Klabu ya Yanga, Arafat Haji, Mwakilishi wa Haier Tanzania, Leon Chi na Mwanasheria anayeiwakilisha kampuni hiyo hapa nchini, Beauttah Camara, wakionyesha jezi zitakazotumiwa na klabu hiyo kwenye Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuingia mkataba wa kuidhamini katika mechi za michuano hiyo. Mkataba huo ulisainiwa juzi usiku jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Haier yaipa nguvu mpya Yanga CAF

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU ikiendelea kujiwinda na mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika ugenini dhidi ya US Monastir ya Tunisia utakaopigwa Februari 11, mwaka huu, Klabu ya Yanga imejazwa nguvu mpya baada ya kuingia mkataba na Kampuni mpya Tanzania ya bidhaa za umeme ya China iitwayo Haier kwa ajili ya michuano hiyo pekee.

Haier imesaini mkataba huo na Yanga juzi usiku, kuwa mdhamini mkuu wa mechi za Kombe la Shirikisho Afrika wenye thamani ya Sh. bilioni 1.5.

Kampuni ya Haier ni namba moja kwa kutengeneza bidhaa bora za umeme majumbani na ofisini, ikiwa na tuzo zaidi ya 500 za ubunifu zenye kuzingatia teknolojia bora na rahisi kwa mtumiaji.

Mkataba huo ulisainiwa mbele ya Rais wa Klabu ya Yanga, Eng. Hersi Said pamoja na mwakilishi wa Kampuni ya Haier, Leon Chi, kwenye hafla fupi iliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Serena, Dar es Salaam.

Haier ambao bidhaa zao kwa hapa Tanzania zitasambazwa na Kampuni ya GSM Group, nembo yao sasa itawekwa mbele kwenye jezi za Yanga watakazotumia kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho pamoja na kupata nafasi kwenye mitandao ya kijamii ya klabu hiyo.

Rais wa Yanga, Hersi amesema ni jambo kubwa kwa Klabu ya Yanga kusaini mka-

INAENDELEA UKURASA 23

# Baleke aiwahi Singida BS

## Aungana na kikosi kambini, Robertinho naye arejea tayari kuiongoza vitani...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikitarajia kuikaribisha Singida Big Stars keshokutwa, Ijumaa kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, habari njema kwa mashabiki wa klabu huyo ni kuwa 'fiti' kwa mshambuliaji wao, Jean Baleke, kushuka dimbani kuwavaa Wakulima wa Alizeti hao.

**Baleke hakuweza kumaliza mchezo uliopita wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup dhidi ya Coastal Union baada ya kugongwa sehemu ya kichwa na kutolewa nje dakika 87 na nafasi yake kuchukuliwa na Augustine Okrah, lakini sasa imeelezwa yupo fiti na tayari kwa mchezo huo wa Ijumaa.**

Kikosi cha Simba kimeingia kambini jana baada ya mazoezi ya asubuhi akiwamo mshambuliaji huyo tayari kujiandaa na mchezo huo dhidi ya Singida Big Stars, utakaochezwa Ijumaa majira ya saa moja usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Baleke yuko fiti na ameungana na wenzake kambini kujiandaa na mchezo huo.

Alisema kikosi kipo imara na wachezaji wote wako tayari kwa ajili ya kumaliza hasira zao baada ya mchezo wa kwanza kudondosha pointi mbili katika Uwanja wa Liti, Singida.

"Kikosi kimeingia kambini na wachezaji wetu wako vizuri kwa ajili ya mchezo huo, tunaingia katika vita ya Ligi Kuu Tanzania Bara, tuna hasira nao, kwa sababu tulitoka sare nyumbani kwao sasa watatueleza ilikuaje.

"Hali ya Baleke iko imara na amefanyiwa vipimo kwa umakini na hajapata shida kubwa katika sehemu ya kichwa na tayari ameshaingia katika mipango ya benchi la ufundi katika mchezo huu," alisema Ahmed.

Aidha, Ahmed aliwataka wanachama wa Simba kuwaunga mkono viongozi wapya waliopo madarakani kwa ajili ya kuifanya Simba iende mbele katika kufikia malengo yao.

"Uchaguzi umekwisha na wale wote ambao kura hazikutosha tunaongeza nguvu moja ili Simba iende mbele, tukiwadhohofisha basi tunaidhohofisha Simba.

Adui yetu ni mpinzani aliyepo katika ligi, yote kwa yote tunaunganisha nguvu zetu kupambana na hao. Kama kuna manung'uniko basi uongozi uliopo madarakani wanatakiwa kuyafanyiwa kazi kwa haraka ili kuondoa masononeko kwa mashabiki," alisema Ahmed.

Kuhusu kurejea kwa Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira, alisema alitarajiwa kuingia jana usiku na leo (Jumatano) atakuwapo kwenye mazoezi ya maandalizi ya mchezo huo utakaochezwa Ijumaa.

"Robertinho atarejea leo usiku (jana), akitoka kwao baada ya kwenda kupata

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >